TANGAZO LA SERIKALI NA. 452 la tarehe 7/7/2023

SHERIA YA UMEME,

(SURA YA 131)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 14(5), 22(1) na 45)*

KANUNI ZA SHUGHULI ZA UZALISHAJI, UPELEKAJI NA USAMBAZAJI UMEME ZA MWAKA 2023
MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA KUOMBA LESENI

4. Wajibu wa kuomba l.eseni.
5. Utaratibu wa kuomba leseni.
6. Kuchapisha ombi la leseni.
7. Kutoa leseni.
8. Maombi ya leseni ya muda
9. Kuchapisha leseni ya muda.
10. Kutoa leseni ya muda.
11. Msamaha.
12. Kuchapisha ombi la kuomba msamaha.
13. Kutoa msamaha.
14. Sababu za maamuzi.
15. Utaratibu wa rufaa.
16. Muda wa kuhamisha leseni.
17. Kusimamisha na kufuta leseni.

SEHEMU YA TATU
WAJIBU WA MWENYE LESENI

18. Mwenye leseni ya kuzalisha umeme.
19. Mwenye Leseni ya kupeleka Umeme.
20. Mwenye leseni ya kusambaza u.meme.
21. Leseni ya biashara ya umeme baina ya nchi na nchi.
22. Wajibu wa jumla wa mwenye leseni.
23. Mkataba wa Huduma kwa Mteja.
24. Fidia kwa hasara iliyopatikana.
25. Ripoti za mwaka.
26. Ripoti ya utendaji.
27. Ukaguzi wa kutii maagizo.
28. Mpango wa kuboresha utendaji.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA FEDHA

29. Utoaji wa taarifa za Fedha.
30. Vigezo vya kutayarisha taarifa za fedha.
31. Uwekaji tofauti wa akaunti za fedha.
32. Kukataza ruzuku kati ya huduma.

SEHEMU YA TANO
MAMBO YA KITAALAM

33. Ukataji Umeme Uliopangwa na matengenezo ya kinga ya mitambo.
34. Kuingilia huduma na matengenezo ya dharura.
35. Notisi ya kuingilia huduma.
36. Uhakika wa huduma ya umeme.
37. Ufungaji wa mita za umeme.
38. Upimaji na uzinduzi.

Sehemu Ndogo ya Pili
Wajibu wa Kitaalam wa Mwenye Leseni ya Kupeleka Umeme

39. Ruhusa na ofa ya kujiunga au kutoa huduma ya upelekaji umeme.
40. Wajibu wa jumla.
41. Haki za mwenye leseni ya upelekaji umeme.
42. Ripoti ya utendaji kazi wa mtandao wa upelekaji umeme.

43. Kupanga mtandao wa upelekaji umeme na upatikanaji wa ardhi.
44. Mpango wa kupanua mtandao wa kupeleka umeme
45. Kipengele cha nguvu ya umeme.
46. Upotevu wa umeme kutokana na upelekaji umeme.
47. Kutii maagizo kutoka kwa mwendeshaji wa soko la umeme.
48. Kuwasilisha taarifa kwa mwendeshaji wa soko la umeme.
49. Matayarisho kukabili dharura.
50. Matengenezo ya kawaida.
51. Matengenezo ya dharura na ukarabati.
52. Matengenezo ya kinga ya mitambo.
53. Kukatisha huduma.
54. Kukatika kwa umeme.
55. Notisi ya kukata huduma.
56. Mita.
57. Mpango wa kuboresha utendaji.
58. Mpango wa kuhakiki ubora.
59.

SEHEMU NDOGO YA TATU
WAJIBU WA KITAALAM WA MWENYE LESENI YA USAMBAZAJI UMEME

60. Huduma za usambazaji umeme.
61. Mkataba wa kusambaza umeme.
62. Mpango wa Mtandao wa Usambazaji na Upatikanaji wa Ardhi
63. Makadirio ya umeme.
64. Ulinzi na usalama wa umeme.
65. Ubora wa huduma.
66. Kipengele cha nguvu ya umeme.
67. Upotevu wa umeme kwenye mtandao na usambazaji.
68. Matayarisho kukabili hali ya dharura.
69. Ukataji umeme uliopangwa na matengenezo ya kinga ya umeme.
70. Kukata umeme na matengenezo ya dharura.
71. Notisi ya kukata huduma ya usambazaji umeme.
72. Ufungaji mita.
73. Kugundua na kuzuia wizi, uharibifu na kuchezea mita.
74. Mpango wa kuboresha utendaji.

SEHEMU YA SITA
UTAMBUZI WA WATEJA MUHIMU

75. Maombi ya kuwa MMeja Muhimu.
76. Vigezo vya uteuzi wa wateja muhimu.
77. Haki za mteja muhimu.
78. Masharti kuwa na nguvu.

SEHEMU YA SABA
UFUATILIAJI NA UTEKELEZAJI

79. Ukaguzi.
80. Wajibu wa Mamlaka wakati wa ukaguzi
81. Vitendo vinavyokatazwa.

SEHEMU YA NANE
MENEJIMENTI YA CHUMBA CHA UDHIBITI

82. Mahitaji ya jumla.
83. Wajibu.
84. Taratibu.
85. Kuzingatia utaratibu wa dharura.
86. Wajibu na majukumu.
87. Taarifa inayotosheleza.
88. Kuhimili uchovu.
89. Menejimenti ya onyo la hatari.
90. Kuthibiti SCADA.
91. Mabadiliko ya Usimamizi.
92. Uzoefu wa uendeshaji.
93. Mpangilio wa chumba cha udhibiti.
94. Mazingira ya joto.
95. Mazingira ya kuona.
96. Hali ya usikivu.
97. Onyo la hatari.
98. Andiko.
99. Lebo.
100. Vifaa vya kuonyeshea.

101. Uthibitisho wa utiifu.
102. Utiifu na kupotoka.

SEHEMU YA TISA
MASHRTI YA JUMLA

103. Mpango wa Kusitisha uendeshaji wa miundombinu ya umeme.
104. Kusitisha uendeshaji wa mitambo wakati wa kufuta leseni.
105. Makosa.
106. Kufuta.

______
JEDWALI
______

SHERIA YA NGUVU ZA UMEME,

(SURA YA 131)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 14(5), 22(1) na 45)*

KANUNI ZA SHUGHULI ZA UZALISHAJI, UPELEKAJI NA USAMBAZAJI UMEME ZA MWAKA 2023

*(Zimetayarishwa chini ya Kifungu cha 14(5), 22(1) na 45)*

SEHEMU YA I
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji wa Umeme za Mwaka 2023.

Matumizi

**2.** Kanuni hizi zitasimamia shughuli za udhiiti zinazohusiana na-

(a) uzalishaji umeme ikiwa ni pamoja na kuzalisha kwa matumizi binafsi, upelekaji, usambazaji na biashara ya shughuli za umeme kati ya nchi na nchi Tanzania Bara.

(b) wateja wanaostahiki; na

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 131

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Umeme;

"mshirika" maana yake ni chombo cha kisheria chenye hisa ndani ya mwenye leseni au chombo cha kisheria kingine ambako mwenye leseni anamiliki hisa;

"onyo la hatari" maana yake ni mfumo unaosikika au unaoonekana unaompa tahadhali mwendeshaji wa

chumba cha udhibiti kuwa kifaa, au mfumo wa uendeshaji una kasoro na ni hatari kulingana na vigezo vya usalama;

Sura ya 414

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji;

"biashara ya umeme kati ya nchi na nchi" maana yake ni biashara ya umeme kati ya nchi mbili zinazopakana kupitia kiunganisha cha umeme, au biashara kati ya nchi mbili zisizokuwa na mipaka ya pamoja, lakini zimeunganika kupitia umeme uliohifadhiwa na nchi hizo kwa ajili ya uuzaji wa nguvu za umeme au ununuzi wa umeme kati ya nchi na nchi;

"chumba cha udhibiti" maana yake ni kituo cha uendeshaji chenye wafanyakazi wenye jukumu la kufuatilia na kudhibiti mfumo wote au vitengo vingi vya miundombinu ya umeme;

"mwendeshaji wa chumba cha udhibiti" ina maana ya mtu mwenye sifa stahiki mwenye jukumu la kufuatilia na kudhibiti usalama wa mfumo wote au vitengo vingi vya miundombinu ya umeme kupitia SCADA iliyofungwa ndani ya chumba cha udhibiti na ambaye ana mamlaka ya uendeshaji na anawajibika na majukumu ya kila siku ya kufuatilia uendeshaji wa miundombinu ya umeme kama inavyofafanuliwa na mwenye leseni;

"mteja" maana yake ni mtu anayepata au kununua huduma zinazodhibitiwa kutoka kwa mwenye leseni;

"kanuni za usambazaji" maana yake ni kanuni za kitaalam na uendeshaji pamoja na vigezo vinavyotolewa na Mamlaka zinazodhibiti shughuli za usambazaji umeme;

"leseni ya usambazaji" maana yake ni idhini inayotolewa na Mamlaka kwa mwenye leseni kuendesha mtandao wa usambazaji;

"mwenye leseni ya usambazaji" maana yake ni chombo kilichopewa leseni na Mamlaka ili kuendesha

mtandao wa usambazaji na ni pamoja na chombo kingine ambacho kimesamehewa kupata leseni ya usambazaji kulingana na kifungu 18 cha Sheria;

"mtandao wa usambazaji" maana yake ni miundombinu ya umeme na vifaa vinavyomilikiwa na mwenye leseni ya usambazaji, kwa madhumuni ya kusambaza umeme wenye nguvu hadi 33kV, na ni pamoja na nyaya za juu, nyaya za chini ya ardhi, transfoma, vituo vya udhibiti na vifaa vya mita za umeme;

"mteja anayestahiki" maana yake ni mtu yeyote aliyeidhinishwa na Mamlaka kwa kutumia kanuni hizi kuingia katika mkataba wa kununua umeme moja kwa moja kutoka kwa mtu mwenye leseni ya kuzalisha umeme;

"kituo" maana yake ni kituo au miundombinu ya umeme iliyojengwa na inakidhi viwango vya kimataifa na ni pamoja na uzalishaji umeme, upelekaji, usambazaji na mfumo wa kushughulikia majanga ya moto wakati shughuli inayodhibitiwa inatekelezwa;

"vifaa vya uzalishaji" maana yake ni majengo, vifaa vya kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na vifaa saidizi, transfoma, vifaa vya kushughulikia mafuta, mtambo wa kubadilishia umeme na kiunganishia umeme ambavyo ni muhimu kwa shughuli za kuzalisha umeme kama zitakavyoelezwa kwenye leseni ya kuzalisha umeme;

"uzalishaji kwa matumizi binafsi" maana yake ni kuzalisha umeme ambao wote utatumiwa na mwenye leseni pasipo kusambaza kwa mtu mwingine;

"leseni ya kuzalisha umeme" maana yake ni idhini iliyotolewa na Mamlaka kwa mtoa huduma kufanya shughuli za kuzalisha umeme;

"mwenye leseni ya kuzalisha umeme" maana yake ni chombo kilichopewa leseni na Mamlaka kutoa huduma ya kuzalisha umeme na ni pamoja na chombo kingine ambacho kimesamehewa kuwa na

leseni ya kuzalisha umeme kulingana na kifungu 18 cha Sheria;

"shughuli za uzalishaji" maana yake ni shughuli za uzalishaji umeme ikiwa ni pamoja na kuzalisha umeme kwa matumizi binafsi na maneno "shughuli ya kuzalisha umeme" yataeleweka hivyo;

"Kanuni za Gridi" maana yake ni kanuni za kitaalam na za kiutaratibu pamoja na viwango vilivyotolewa na Mamlaka ili kudhibiti shughuli za **upelekaji** umeme na mfumo wa uendeshaji;

"mkaguzi" maana yake ni afisa wa Mamlaka au wakala aliyeteuliwa na Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 31(2) cha Sheria kufanya kazi kama mkaguzi;

"sehemu ya kuunganishia umeme" maana yake ni andiko la nia kutoka kwa mwenye leseni ya usambazaji umeme kutaka kujiunga na kununua umeme wa mpaka megawati 10 utakaozalishwa na mwekezaji;

"barua ya kuonyesha nia" maana yake ni andiko la nia kutoka kwa mwenye leseni ya usambazaji umeme kutaka kujiunga na kununua umeme wa mpaka megawati 10 utakaozalishwa na mwekezaji;

"leseni" maana yake ni leseni ya biashara ya umeme kati ya nchi na nchi, leseni ya kuzalisha umeme, leseni ya kupeleka umeme au leseni ya kusambaza umeme iliyotolewa na Mamlaka;

"mwenye leseni" maana yake ni mmiliki wa leseni ya biashara ya umeme kati ya nchi na nchi, leseni ya kuzalisha umeme, leseni ya kupeleka umeme au leseni ya kusambaza umeme;

"leseni ya miundombinu ya umeme" ina maana ya majengo, vifaa vya kuzalisha umeme, kupeleka umeme na/au kusambaza umeme pamoja na vifaa saidizi, transfoma, vifaa vya kushughulikia mafuta, mtambo wa kubadilishia umeme na vifaa vya kuunganishia umeme ambavyo ni muhimu kwa shughuli za kuzalisha umeme kama

zinavyotamkwa kwenye leseni husika;

Sura ya 287 na 288

"mamlaka ya serikali za mitaa" maana yake ni mamlaka ya wilaya, mamlaka ya mji, mamlaka ya kata au mamlaka ya kijiji kama zilivyoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"Waziri2 maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya umeme;

"mkataba wa ununuzi umeme" maana yake ni mkataba wa kununua na kuuza umeme ulioingiwa kati ya mzalisha umeme na mhusika mwingine;

"leseni ya muda" ina maana ya leseni iliyotolewa na Mamlaka kumruhusu mwombaji kufanya matayarisho ya shughuli mbalimbali kama za uchunguzi, utafiti na shughuli nyingine muhimu kwa ajili ya kuomba leseni;

"Matendo Bora ya Utoaji Huduma" ina maana ya matendo mazuri na bora, mbinu na utaratibu ambao unapatikana kwa kutumia ujuzi, bidii, busara na kubashiri yaliyo mbeleni mbayo kwa kawaida yanatarajiwa kupatikana kutoka kwa mtaalam mbobezi mwendeshaji wa kimataifa anayefanya kazi hizo au shughuli inayofanana na inayodhibitiwa ndani ya Tanzania na ambayo iko chini ya mazingira yanayofanana na yanakidhi matakwa ya kitaifa na kimataifa ya kiafya, usalama na mazingira;

"shughuli inayodhibitiwa" ina maana ya biashara ya umeme kati ya nchi na nchi, shughuli ya kuzalisha umeme, kupeleka umeme au shughuli ya kusambaza umeme na maneno "huduma zinazodhibitiwa" yataeleweka hivyo;

"ripoti za fedha zinazodhibitiwa au taarifa za fedha zinazodhibitiwa" ina maana ya taarifa za fedha au ripoti zilizotayarishwa na kuwasilishwa kwa Mamlaka na chombo kinachodhibitiwa kama inavyoelekezwa kwenye miongozo ya kutayarisha taarifa za fedha zinazothibitiwa;

"SCADA" ina maana ya mfumo unaotumia kompyuta au mfumo ambao unakusanya na kuonyesha taarifa kuhusu miundombinu ya umeme na una uwezo wa kutuma maagizo kwenda kwenye miundombinu ya umeme au mfumo ambao unajumuisha vifaa vya kompyuta na "software" inayotumiwa kupeleka maagizo na kupata takwimu kwa madhumuni ya kufuatilia na kudhibiti miundominu ya umeme;

"eneo" ina maana ya mahali ambako miundombinu ya uzalishaji imewekwa na taarifa yake itatolewa kwenye leseni;

"mradi mdogo wa umeme" maana yake ni mtambo wa umeme unaotumia nishati mbadala au nishati jadidifu kuzalisha umeme wa hadi Megawati 10;

"bei" maana yake ni tozo yoyote, ada, bei au kiwango cha bei kwa madhumuni ya kununua huduma inayodhibitiwa na ambayo imeidhinishwa na Mamlaka;

"mbinu ya upangaji bei" maana yake ni njia inayotumika kupanga bei kama ilivyoidhinishwa na Mamlaka;

"leseni ya kupeleka umeme" maana yake ni idhini inayotolewa na Mamlaka kwa mtoa huduma kuendesha mtandao wa upelekaji umeme;

"mwenye leseni ya kupeleka umeme" maana yake ni chombo kilichopewa leseni na Mamlaka kuendesha mtandao wa upelekaji umeme na ni pamoja na chombo kingine ambacho kimesamehewa kupata leseni ya kupeleka umeme kulingana na kifungu 18 cha Sheria;

"mtandao wa upelekaji umeme" maana yake ni mkusanyiko wa vifaa na miundombinu ya umeme inayomilikiwa na mwenye leseni ya upelekaji umeme ili kupeleka umeme na nguvu ya umeme wa 50Hz kwa kutumia nyaya za msongo wa umeme wa 66kv na zaidi ambao ni pamoja na nyaya za juu, nyaya za chini ya ardhi, nyaya za majini, transfoma, mtandao wa mawasiliano, vituo

vya udhibiti na vifaa vya kufungia mita za umeme; na

"mkataba wa kupeleka umeme" maana yake ni mkataba wa kupeleka nguvu ya umeme kutoka kwenye chanzo cha umeme kilichounganishwa na gridi ya umeme kwenda kwenye kituo cha umeme ndani ya gridi.

## SEHEMU YA PILI
## UTARATIBU WA KUOMBA LESENI

Wajibu wa kuomba leseni

4.- (1) Mtu hataweza kutoa huduma inayodhibitiwa pasipo kuwa na leseni.

(2) Mtu anayekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Utaratibu wa kuomba leseni

5.-(1) Mtu atawasilisha maombi ya leseni kwa Mamlaka kama itakavyoelekezwa na Mamlaka na maombi hayo yataambatana na nyaraka zifuatazo:

(a) nakala halisi ya nyaraka za usajili wa mwombaji;
(b) ushahidi wa malipo ya ada ya maombi;
(c) vyeti vya usajili vya Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi na Kodi ya Ongezeko la Thamani;
(d) chanzo cha fedha za mradi;
(e) nakala halisi ya cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira na jamii; na
(f) taarifa yoyote nyingine kama itakavyohitajika na Mamlaka

(2) Pamoja na taarifa zilizotajwa kwenye kanuni ndogo ya n(1),maombi ya leseni yataambatana na yafuatayo:

(a) kwa leseni ya uzalishaji umeme- barua ya kuunga mkono maombi kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya umeme;

(i) ushahidi wa kuunga mkono mradi kutoka mamlaka ya serikali za mitaa;

(ii) ushahidi wa haki ya kutumia maji kwa waombaji wanaotaka kuzalisha umeme kwa kutumia maji;

(iii) ushahidi wa haki ya kutumia ardhi kuweka miundombinu ya umeme;

(iv) ushahidi wa kupewa idhini ya kuendeleza eneo ikiwa ni pamoja na kibali cha ujenzi;

(v) ripoti ya upembuzi yakinifu;

(vi) mkataba wa ununuzi wa umeme pale inapohusika;

(vii) ramani ya eneo;

(viii) maelezo ya vifaa vya kuzalishia umeme;

(ix) michoro ya ujenzi utakavyokuwa; na

(x) ripoti ya utendaji kazi

kwa leseni ya upelekaji umeme-

(b) ushahidi wa kuwepo kwa umeme wa kupeleka pamoja na mkataba wa ununuzi, leseni ya kuagiza umeme;

(i) maelezo ya eneo la huduma;

(ii) maelezo ya mtandao wa upelekaji umeme;

(iii) ushahidi wa kupata haki ya njia ya umeme;

(iv) ripoti ya upembuzi yakinifu;

(v) mpango wa kupanua mtandao wa upelekaji umeme kama upo;

a. michoro ya ujenzi utakavyokuwa; na

(vi) ripoti ya utendaji kazi.

(c) kwa leseni ya kusambaza umeme-

(i) barua ya kuunga mkono maombi kutoka kwa Wizara yenye dhamana

na masuala ya umeme;

(ii) ushahidi wa kuunga mkono mradi kutoka mamlaka za serikali za mitaa;

(iii) ushahidi wa kuwepo kwa umeme wa kusambaza;

(iv) ripoti ya upembuzi yakinifu;

(v) maelezo ya eneo linalotakiwa kusambaziwa umeme;

(vi) maelezo ya mtandao wa usambazaji umeme;

(vii) mpango wa upanuzi huduma kama upo;

(viii) michoro ya ujenzi utakavyokuwa; na

(ix) ripoti ya utendaji kazi.

(i) kwa ajili ya biashara ya umeme kati ya nchi na nchi-

(ii) mkataba wa ununuzi wa umeme;

(iii) mkataba wa kuunganisha umeme

(iv) mkataba wa ushirikiano baina ya nchi husika, kama upo; na

(v) mkataba wa kupeleka Umeme pale inapohusika.

(3) Maombi ya leseni yataambatana na ada ya maombi isiyoweza kurejeshwa kama inavyoelezwa na Mamlaka.

(4) Bila kujali masharti ya Kanuni hizi, maombi ya leseni ya upelekaji umeme yatafanywa tu na kampuni ya kupeleka umeme inayomilikiwa na Serikali.

Kuchapisha maombi ya leseni

6.-(1) Maombi ya leseni yaliyopokelewa na Mamlaka yatachunguzwa ili kubaini usahihi wake na uhalali wa taarifa zilizotolewa na baadaye notisi ya maombi hayo itachapishwa angalau kwenye magazeti mawili yanayosambazwa sana nchini Tanzania, moja la Kingereza na lingile la Kiswahili kwa madhumuni ya

kupata maoni na uwakilishi juu ya mombi.

(2) Umma utakaribishwa kutoa maoni na uwakilishi ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe ya kuchapisha notisi na maoni na uwakilishi uliotolewa utatumiwa na Mamlaka katika kufikia uamuzi juu ya mombi.

7.-(1) Mamlaka, baada ya siku ishirini na moja kumalizika itafanya tathmini ya mombi la leseni ili iweze kuamua-

(a) kuidhinisha ombi na kutoa leseni;
(b) kurudisha ombi kwa rejea zaidi; au
(c) kutoa msamaha wa kutokuwa na leseni.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), leseni ya kupeleka umeme itatolewa tu kwa kampuni ya kupeleka umeme inayomilikiwa na Serikali.

(3) Mamlaka wakati wa kufanya uamuzi wa kama kutoa leseni, kukataa au kutoa msamaha, itazingatia mambo yafuatayo:

(a) kukinga uharibifu wa mazingira;
(b) ufanisi kiuchumi na faida kwa mwombaji na umma kwa ujumla;
(c) maoni na uwakilishi uliopokelewa kutoka kwa wananchi, kama upo;
(d) kama miundombinu ya umeme inakidhi matakwa yafuatayo:
   (i) usalama;
   (ii) afya;
   (iii) ulinzi;
   (iv) vitu hatari;
   (v) mazingira;
   (vi) mahitaji ya mipango ya kijijini na mijini, na;
(e) jambo lolote muhimu linalohusika na utoaji wa busara wa huduma ya biashara ya umeme baina ya nchi husika,

uzalishaji umeme, kusambaza umeme au huduma ya kupeleka umeme nchini Tanzania.

Kutoa leseni

(4) Ikiwa leseni iliyotolewa chini ya kanuni hii itakwisha muda wake, mwenye leseni anaweza kuomba upya au kuongezewa muda wa leseni kama itakavyoelekezwa na Mamlaka.

(5) Maombi ya kuomba upya au kuongezewa muda wa leseni yataambatana na taarifa husika au nyaraka kama Mamlaka itakavyohitaji.

Maombi ya leseni ya muda

8.-(1) Mtu anayetaka kutoa huduma inayodhibitiwa anaweza, kabla ya kuomba leseni, kuwasilisha kwenye Mamlaka ombi la kupewa leseni ya muda kwa madhumuni ya kufanya uchunguzi na tathmini mbalimbali na kufanya mipango ya fedha na shughuli nyingine muhimu kwa ajili ya kuomba leseni.

(2) Maombi ya leseni ya muda yatawasilishwa kwenye Mamlaka kwa kutumia mfumo ambao umeelezwa na Mamlaka na utaambatana na:

(a) nakala halisi za nyaraka za usajili wa mwombaji;

(b) ushahidi wa malipo ya ada ya maombi;

(c) mpango wa fedha wa mradi;

(d) vyeti vya usajili wa TIN na VAT;

(e) nakala halisi ya cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira na jamii au idhini kama inavyotakiwa na Sheria ya Menejimenti ya Mazingira au ushahidi wa kuanza mchakato wa kupata cheti au idhini; na

(3) Mwombaji pamoja na nyaraka zilizotajwa kwenye kanuni ndogo (2) atatakiwa kuwasilisha yafuatayo:

(a) kwa leseni ya kuzalisha umeme:

(i) ramani ya eneo;

(ii) teknolojia ya uzalishaji na uwezo

wake;
(iii) utaratibu wa ujenzi;
(iv) barua ya kuunga mkono ombi kutoka Wizara inayoshughulikia umeme;
(v) ushahidi wa kuunga mkono mradi kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
(vi) ushahidi wa haki ya kutumia maji kwa waombaji wanaotaka kuzalisha umeme kwa kutumia maji, kama upo;
(vii) ushahidi wa haki ya kutumia ardhi kwa ajili ya mradi au kuanza mchakato wa kupata haki hiyo;
(viii) ushahidi wa kupewa idhini ya kuendeleza eneo ikiwa ni pamoja na kibali cha ujenzi, kama kipo;
(ix) ripoti ya awali ya upembuzi yakinifu au taarifa ya mradi; na
(x) mkataba wa ununuzi wa umeme, mkataba wa makubaliano, au barua ya kusudio, yoyote inayohusika.

(b) kwa leseni ya upelekaji umeme:
(i) ushahidi wa kuwepo nguvu za umeme wa kupeleka pamoja na mkataba wa ununuzi, leseni ya kuagiza umeme au mkataba wa kupeleka umeme;
(ii) maelezo ya eneo la huduma;
(iii) maelezo ya mtandao wa upelekaji umeme;
(iv) ushahidi wa kupata haki hiyo;
(v) utaratibu wa ujenzi;
(vi) ripoti ya awali ya upembuzi yakinifu;
(vii) mpango wa kupanua

mtandao wa upelekaji umeme, kama upo;

(viii) ramani ya eneo la kutolea huduma.

(c) Kwa leseni ya kusambaza umeme:

(i) barua ya kuunga mkono ombi kutoka kwa Wizara inayoshughulikia umeme;

(ii) ushahidi wa kuunga mkono mradi kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(iii) ushahidi wa kuwepo kwa umeme wa kusambaza;

(iv) ripoti ya awali ya upembuzi yakiniifu;

(v) maelezo ya eneo linalotakiwa kusambaziwa umeme;

(vi) maelezo ya mtandao wa usambazaji;

(vii) haki ya njia ya umeme au mchakato wa kupata haki hiyo;

(viii) utaratibu wa ujenzi; na

(ix) mpango wa upanuzi, kama upo.

Kuchapisha maombi ya leseni ya muda

9.-(1) Maombi ya leseni ya muda yaliyopokelewa na Mamlaka yatafanyiwa tathimini ili kubaini usahihi na uhalali wa taarifa zilizotolewa na baadaye notisi ya ombi hilo itachapishwa angalau kwenye magazeti mawili yanayosambazwa sana nchini Tanzania, moja la Kingereza na lingine la Kiswahili kwa madhumuni ya kupata maoni na uwakilishi juu ya ombi.

(2) Umma utakaribishwa kutoa maoni na uwakilishi ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe ya kuchapisha wa notisi na maoni na uwakilishi uliotolewa utatumiwa na Mamlaka katika kufikia uamuzi juu ya maombi.

Kutoa leseni ya

10.-(1) Mamlaka, baada ya siku inshirini na

muda

moja kumalizika itafanya tathmini ya maombi ya leseni na kuamua kulingana na-

(a) ufanisi kiuchumi na faida kwa mwombaji na umma kwa ujumla; na

(b) maoni na uwakilishi uliopokelewa kutoka kwa wananchi, kama upo.

(2) Ikiwa leseni iliyotolewa chini ya kanuni hii itakwisha muda wake, mwenye leseni anaweza kuomba upya au kuongezewa muda wa leseni kama inavyoelezwa na Mamlaka.

(3) Maombi ya kuomba upya au kuongezewa muda wa leseni ya muda wa leseni ya muda yataambatana na taarifa husika au nyaraka kama Mamlaka itakavyohitaji.

Msamaha

11.-(1) Mtoa huduma yeyote anayetoa huduma au ana nia ya kutoa huduma inayodhibitiwa lakini ana sababu za kutosha za kutokuzingatia matakwa ya leseni anaweza kuomba kwa Mamlaka asamehewe kutotekeleza masharti ya kifungu cha 8 cha Sheria.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1) mtu yeyote anayefanya yafuatayo:

(a) kutumia mitambo ya kuzalisha umeme yenye uwezo chini ya megawati moja; au

(b) kusambaza umeme ulio nje ya gridi kwenye maeneo ya vijiji ambako mahitaji ya juu ya umeme nje ya gridi ni chini ya megawati moja,

(c) atapewa msamaha wa kutozingatia masharti ya kifungu cha 8 cha Sheria.

(3) Maombi ya msamaha chini ya kanuni ndogo ya (1) yatafanywa kwa maandishi kwenda kwa Mamlaka yakieleza yafuatayo:

(a) maelezo ya mradi pamoja na wamiliki wake, maelezo ya mitambo, maelezo ya eneo la mradi na

mapendekezo ya eneo la kutoa huduma; na

(b) sababu za kuomba kupewa msamaha.

(4) Mtu aliyepewa msamaha wa kutofuata masharti ya kifungu cha 8 cha Sheria atatakiwa kujisajili na Mamlaka na kuipatia Mamlaka taarifa sahihi kuhusiana na huduma za kuzalisha umeme au kusambaza umeme.

(5) Isipokuwa kama inahitajika na Mamlaka, shughuli za uzalishaji umeme wenye uwezo chini ya megawati moja na ni kwa matumizi binafsi zitasamehewa na mahitaji ya kujisajili.

Kuchapisha maombi ya kuomba msamaha

12.-(1) Baada ya kupokea maombi yaliyofanyika kwa mujibu wa kanuni ya 11, Mamlaka itachapisha notisi ya maombi angalau kwenye magazeti mawili yanayosambazwa sana nchini Tanzania, moja la Kishwahili na moja la Kiingereza kwa madhumuni ya kupata amaoni na uwakilishi juu ya maombi.

(2) Umma utakaribishwa kutoa maoni na uwakilishi ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe ya kuchapisha notisi na maoni na uwakilishi uliotolewa utatumiwa na Mamlaka katika kufikia maamuzi juu ya maombi.

Kutoa msamaha

13.- (1) Mamlaka, baada ya siku ishirini na moja kumalizika itafanya tathmini ya maombi na kufanya uamuzi wa kama kutoa msamaha au kukataa maombi chini ya masharti mbalimbali kama itakavyo onekakana inafaa.

(2) Mamlaka, wakati wa kuamua kama kutoa au kukataa maombi ya msamaha, itazingatia yafuatayo:

(a) uzito wa sababu zilizowasilishwa kuunga mkono ombi la msamaha;

(b) kulinda maslahi ya umma; na

(c) maoni au uwakilishi uliopokelewa kutoka kwa wananchi, kama yapo.

Sababu za maamuzi

14.- Mamlaka, ikitokea kuwa inakataa ombi la leseni au kurudisha ombi hilo kwa rejea zaidi, au kukataa ombi la msamaha, itamfahamisha mwombaji kuhusu uamuzi huo kwa maandishi, ikiwa ni pamoja na sababu za kufanya hivyo.

Utaratibu wa rufaa
Sura ya 285

15. Mtu ambaye hataridhika na maamuzi ya Mamlaka anaweza kukata rufaa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ushindani.

Muda wa kuhamisha leseni

16.-(1) Masharti ya leseni na leseni ya muda yatabainishwa juu ya leseni au leseni ya muda, kama itakavyoonekana.

(2) Leseni itaendelea kutumika katika muda uliotamkwa isipokuwa, Mamlaka kufuatia ombi la mwenye leseni itaongeza muda wa leseni kama Mamlaka itakavyoona inafaa.

(3) Leseni au leseni ya muda haitapewa au kuhamishwa kwenda kwa mtu mwingine pasipo idhini ya maandishi kutoka kwenye Mamlaka.

(4) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (3), mabadiliko ya umiliki ambapo chombo kingine kinakuwa mmiliki wa hisa nyingi kwenye shughuli za mwenye leseni, ambako leseni au leseni ya muda imetolewa, hali hii inatakiwa kutolewa taarifa kwa Mamlaka ndani ya siku kumi na nne baada ya kupata idhini za kuhamisha leseni kutoka Mamlaka husika.

Kusimamisha na kufuta leseni

17.-(1) Mamlaka inaweza kusimamisha matumizi ya leseni kwa kipindi hadi miezi kumi na mbili ikiwa kumetokea-

(a) ukiukwaji wa masharti ya leseni; au

(b) ukiukwaji wa masharti ya Sheria, Kanuni hizi au sheria husika;

(c) mwenye leseni ameshindwa kulipa

tozo ya udhibiti kwa Mamlaka na tozo hiyo imebaki haijalipwa kwa siku thelathini baada ya siku ambayo ilitakiwa kulipwa na Mamlaka kumpa mwenye leseni notisi kwa maandishi kuwa malipo hayo yamechelewa.

(2) Mamlaka inaweza kufuta leseni ambapo itaamua kuwa mwenye leseni ameshindwa kurekebisha au kujizuia kutenda kosa linaloashiria uvunjaji wa masharti ndani ya muda uliowekwa pamoja na kuelezwa kufanya hivyo na Mamlaka.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) Mamlaka inaweza-

(a) kusamehe kusimamishwa kwa leseni kama imeridhika kuwa mwenye leseni amejizuia na matendo yaliyo sababisha leseni yake kusimamishwa na sababu za kufanya hivyo hazipo tena; na

(b) badala ya kusimamisha au kufuta leseni kwa mujibu wa masharti ya Sheria, kuteua msuluhishi kulingana na miongozi inayotolewa na Mamlaka, ili kubadilisha menejimenti ya mwenye leseni na kuanza kushughulikia mambo yake katika kipindi ambacho Mamlaka itakiona kinafaa.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU WA MWENYE LESENI

Mwenye leseni ya kuzalisha umeme

18.-(1) Mwenye leseni ya kuzalisha umeme anatakiwa kufanya yafuatayo:

(a) kutoa huduma za kuaminika za kuzalisha umeme kwa wateja;

(b) kuendesha na kuhifadhi miundombinu ya kuzalisha umeme;

(c) kutoza wateja bei iliyoidhinishwa; na

(d) kufanya shughuli zote zinazohusika na

utoaji huduma za kuzalisha umeme, ikiwa ni pamoja na uhandisi, ujenzi, ukarabati, uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya uzalishaji umeme kulingana na matendo bora na ya busara ya utendaji na mkataba wa ununuzi umeme.

(2) Mwenye leseni ya kuzalisha umeme anaweza kutumia sehemu ya umeme anaozalisha kukidhi mahitaji yake ya umeme.

Mwenye leseni ya upelekaji umeme

19.-(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atatakiwa kufanya yafuatayo:

(a) kufanya shughuli ya upelekaji umeme katika eneno la kutolea huduma;

(b) kuendesha na kuhifadhi mtandao wa upelekaji umeme;

(c) kutoza wateja bei iliyoidhinishwa au kufuatana na sheria husika;

(d) kufanya shughuli zote zinazohusika na upelekaji umeme, ikiwa ni pamoja na uhandisi, ujenzi, ukarabati, uendeshaji na matengenezo ya miundo mbinu ya upelekaji umeme kulingana na sheria husika na matendo bora na ya busara ya utendaji;

(e) kuruhusu matumizi ya miundombinu ya kupeleka umeme na kutoa shughuli za upelekaji umeme kwa watu wenye ujuzi pasipo upendeleo; na

(f) kuchapisha utaratibu unaotumika katika kuomba kuunganishwa kwenye miundombinu ya upelekaji umeme.

Mwenye leseni ya usambazaji umeme

20. Mwenye leseni ya usambazaji umeme atatakiwa kufanya yafuatayo:

(a) kufanya shughuli za usambazaji katika eneo la kutolea huduma;

(b) kuendesha na kuhifadhi mtandao wa usambazaji umeme;

(c) kutoza wateja bei iliyoidhinishwa;

(d) kufanya shughuli zote zinazohusika na usambazaji umeme, ikiwa ni pamoja na uhandisi, ujenzi, ukarabati, uendeshaji na matengenezo ya miundombinu kulingana na sheria husika na matendo bora na ya busara ya utendaji; na

(e) pale inapowezekana, kununua umeme unaohitajika kwanza kutoka kwa mzalishaji umeme mwenye gharama ndogo za uzalishaji.

Mwenye leseni ya biashara ya umeme baina ya nchi na nchi

21.-(1) Mwenye leseni ya biashara ya umeme baina ya nchi na nchi anatakiwa kufanya yafuatayo:

(a) kufanya shughuli za biashara ya umeme kati ya nchi na nchi katika mfumo ambao hauathiri usalama wa gridi ya Taifa;

(b) kuifahamisha Mamlaka kama kuna mabadiliko yoyote kwenye mkataba wa biashara ya umeme baina ya nchi na nchi ambayo yataleta mabadiliko katika bei iliyoidhinishwa;

(c) kuwasilisha kwenye Mamlaka kila mwaka ripoti ya ukaguzi wa mahesabu na utendaji;

(d) kuwasilisha kwenye Mamlaka kupata idhini ya Mamlaka, Mkataba wa Ununuzi wa Umeme, Mkataba wa Kupeleka Umeme na tozo na bei zinazohusika.

(2) Mamlaka inaweza kutayarisha miongozo ya kufanikisha biashara ya umeme baina ya nchi na nchi.

Wajibu wa jumla wa mwenye leseni

22. Mwenye leseni, pale inapohusika wakati wa kutoa huduma inayodhibitiwa, kuzingatia kanuni na miongozo inayotolewa na Mamlaka na-

(a) kutoza bei iliyoidhinishwa na Mamlaka;
(b) kulipa ada na tozo zinazohusika;
(c) kutoa huduma inayodhibitiwa pasipo ubaguzi na upendeleo kwa wateja;
(d) kutoacha kutoa huduma inayodhibitiwa pasipo kutoa notisi kwanza kwa Mamlaka; na
(e) kuifahamisha Mamlaka kuhusu ajali zinazotokea wakati wa kutoa huduma ndani ya saa 24 kwa ajali mbaya na kila mwaka kwa ajali za kawaida.

Mkataba wa Huduma kwa Mteja

23. Mwenye leseni ya usambazaji wa umeme ndani ya miezi mitatu kutoka tarehe ya kupewa leseni au uhamisho wa leseni, atatayrisha na kuwasilisha kwenye Mamlaka kwa kuidhinishwa mkataba wa huduma kwa mteja ambao utakuwa na:
(a) ofa ya kuunga au kutoa huduma kwa mteja baada ya kupokea ombi kutoka kwa mteja huyo;
(b) ofa ya kuunga mzalishaji wa umeme mwenye leseni, ikiwa ni pamoja na miradi midogo ya kuzalisha umeme kulingana na utaratibu ulioidhinishwa na Mamlaka;
(c) wajibu wa mwenye leseni na ule wa mteja na usuluhisho kwa kukiuka wajibu; na
(d) kiwango cha chini cha ubora wa utoaji huduma za umeme na viwango husika kulingana na matendo bora na ya busara ya utendaji.

Fidia kwa hasara Iliyopatikana

24.-(1) Mwenye leseni atawajibika kumlipa fidia mtu yeyote ambaye ameumia au kupoteza mali zake kutokana na huduma inayodhibitiwa.

(2) Mtu ambaye ameumia au kupoteza mali zake kutokana na huduma inayodhibitiwa, kwanza atawasilisha malalamiko yake kwa mwenye leseni kwa

mategemeo ya kufikia suluhisho.

(3) Endapo hakuna suluhisho lililofikiwa chini ya kanuni ndogo ya (2), mtu ambaye ameumia au kupoteza mali atawasilisha jambo hilo kulingana na matakwa ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji.

(4) Kwa madhumuni ya kanuni hii, mtu inajumuisha msuluhishi au msuluhishaji, mtekelezaji au msimamizi/wasii wa mali za mtu aliyekufa.

Ripoti za Mwaka

25.-(1) Mwenye leseni atawasilisha kwenye Mamlaka ripoti ya mwaka sio zaidi ya siku thelathini baada ya kutoa mahesabu yaliyo kaguliwa.

(2) Ripoti ya mwaka iliyotayarishwa na mwenye leseni na kuwasilishwa
kwenye Mamlaka itatoa taarifa kuhusu mambo ya kitaalam na kiuchumi ya shughuli zinazodhibitiwa ambazo zimetekelezwa kwa mwaka mzima.

Ripoti ya utendaji

26. Mwenye leseni kila mwezi au wakati wowote mwingine kama Mamlaka itakavyohitaji, atatoa ripoti ya utendaji kazi katika shughuli zake zote zinazodhibitiwa katika namna itakayotolewa na Mamlaka na repoti hizo zitakuwa zinawasilishwa kwa Mamlaka ndani ya siku saba za mwezi unaofuata.

Ukaguzi wa kutii maagizo

27.-(1) Mamlaka kila mwaka itafanya ukaguzi wa kila mwenye leseni ili kubaini kama wanatii masharti kwenye mambo yafuatayo:

(a) Kanuni hizi;

(b) mikataba ya ununuzi umeme, mkataba wa shughuli za kuzalisha umeme, upelekaji umeme au usambazaji umeme; na

(c) malengo husika.

(2) Mamlaka inaweza, kama itaona ni muhimu kufanya hivyo, kumteua mkaguzi kufanya ukaguzi ulioelezwa kwenye kanuni ndogo ya (1).

Mpango wa kuboresha utendaji

28. Mwenye leseni ambaye utendaji wake uko chini ya viwango husika, kila mwaka, atawasilisha

kwenye Mamlaka mpango wa kuboresha utendaji kazi wake ukijumuisha vigezo muhimu vya utendaji kazi kulingana na:

(a) vigezo bora vya kimataifa;

(b) Matendo Bora na Busara ya Utendaji; na

(c) maagizo yanayotolewa na Mamlaka

SEHEMU YA NNE
MASHAETI YA FEDHA

Utoaji wa taarifa za fedha

29.-(1) Mwenye leseni ndani ya siku tisini baada ya kuanza mwaka wa fedha atawasilisha kwa Mamlaka bajeti ya mwaka wake wa fedha kulingana na shughuli zinazodhibitiwa na bajeti hiyo itakujumuisha yafuatayo:

(a) fedha za uendeshaji; na

(b) gharama za uwekezaji na gharama za uendeshaji.

(2) Mwenye leseni kila mwaka atawasilisha kwenye Mamlaka yafuatayo:

(a) ripoti ya fedha ndani ya siku tisini (90) tangu mwisho wa mwaka wa fedha; na

(b) hesabu zilizokaguliwa ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupokea mahesabu hayo.

Vigezo vya kutoa taarifa ya fedha

30.-(1) Mwenye leseni atawasilisha ripoti za taarifa ya fedha za udhibiti kulingana na vigezo vilivyowekwa na Mamlaka.

(2) Vigezo vya kutoa taarifa ya fedha za udhibiti na marudio ya utoaji taarifa utakuwa kama inavyoelezwa kwenye mwongozo wa kutoa taarifa za fedha za udhibiti.

Uwekaji Tofauti wa Akaunti za Fedha

31.-1) Mwenye leseni atakuwa akaunti tofauti za fedha kwa ajili ya kutoa huduma ambazo hazihusiani na shughuli inayodhibitiwa.

(2) Mwenye leseni ambaye ana leseni zaidi ya moja atakuwa na vitabu tofauti vya fedha na atawajibika kuwasilisha taarifa tofauti kwa kila leseni.

(3) Masharti ya kanuni ndogo ya (2) hayatahusika kwa mwenye leseni ambaye anafanya shughuli zote mwenyewe ndani ya kampuni mpaka hapo soko la umeme limefanyiwa marekebisho kulingana na kifungu cha 41 cha Sheria.

Kukataza ruzuku kati ya huduma

32.Mwenye leseni atahakikisha kuwa hakuna ruzuku kati ya-

(a) shughuli zinazodhibitiwa; au

(b) shughuli zinazodhibitiwa na shughuli nyingine yoyote ikiwa ni pamoja na shughuli za washirika.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA KITAALAM

Ukataji umeme uliopangwa na matengenezo ya Kinga ya mitambo

33. Mwenye leseni ya kuzalisha umeme atafanya yafuatayo:

(a) atafanya shughuli za matengenezo ya kinga ya mitambo kama inavyohitajika kulingana na masharti ya watengenezaji kuhakikisha kuwa huduma za uzalishaji umeme ni endelevu na za uhakika; na

(b) kutoa taarifa ya ukataji umeme uliopangwa kutokea kwa Mamlaka kwa maandisi si chini ya siku tisini kabla ya tukio hilo kutokea.

Kuingilia huduma na matengenezo ya dharura

34. Mwenye leseni ya kuzalisha umeme atafanya yafuatayo-

(a) kuchukua hatua stahiki za kurudisha

huduma ya kuzalisha umeme endapo itagundulika kuwa upatikanaji umeme kwa mteja kutoka kwenye kiungio cha umeme umepunguzwa au kuingiliwa kwa sababu yoyote ile isipokuwa kukatika kwa umeme kitendo ambacho hakikupangwa;

(b) baada ya kuambiwa kuhusu uharibifu wa mitambo au vifaa ambao unasababisha hatari au maumivu au hasara kwa mali, kuondoa hatari hiyo au maumivu hayo mara moja kabla ya matengenezo ya dharura au ukarabati wa mitambo; na

(c) mara moja kufanya matengenezo ya mtambo ulioharibika au vifaa na dosari nyingine kwenye miundombinu ya kuzalisha umeme na mara moja baadaye kuzindua uendeshaji wa mitambo au vifaa hivyo.

Notisi ya kuingilia huduma

35. Mwenye leseni ya kuzalisha umeme atafanya:ndani ya saa ishirini na nne-

(a) ndani ya siku saba kabla ya ukataji umeme uliopangwa kutokea kuifahamisha Mamlaka na wateja kwa maandishi ikiwa huduma ya uzalishaji umeme itaingiliwa kwa madhumuni ya kufanya ukarabati, matengenezo ya kinga ya mitambo au kwa sababu yoyote nyingine nje ya uwezo wa mwenye leseni ya uzalishaji umeme, na

(b) kuwafahamisha wateja na kutoa taarifa mapema kwenye Mamlaka kwa maandishi endapo huduma ya kuzalisha umeme itaingiliwa kwa madhumuni ya kufanya matengenezo ya dharura au kwa sababu yoyote nyingine nje ya uwezo wa mwenye leseni, kama kuingiliwa kwa huduma ya umeme kunaathiri utoaji

huduma za kuzalisha umeme kwa zaidi ya saa ishirini na nne.

Uhakika wa huduma ya umeme

36. Mwenye leseni ya kuzalisha umeme atahakikisha kuwa, tangu kuanza kutumika kwa leseni, na kwa wakati mwingine baadaye hadi kuisha muda wa leseni yake, anapokea kwa uhakika malighafi zinazotakiwa katika shughuli za kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na vipuri, mafuta na maji yene ubora unaotakiwa na idadi ya kutosha kukidhi mahitaji ya nguvu za umeme.

Ufungaji mita

37. Mwenye leseni ya kuzalisha umeme atafanya yafuatayo:

(a) atafunga mita kupima umeme na rasilimali nyingine zinazotakiwa kuzalisha umeme, kulingana na kanuni na utaratibu wa upimaji na vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba ulioingiwa kati ya mwenye leseni na mtu mwingine;

(b) kuhakikisha kuwa mita za umeme zina usahihi uliokubalika na hautakiwi kuzidi asilimia 0.5;

(c) kuthibitisha usahihi na marekebisho ya mita na kuhakikisha mita zote zinatoa taarifa sahihi isipokuwa pale ambapo mkataba wa ununuzi wa umeme unatamka vinginevyo;

(d) kuchukua hatua stahiki kuzuia kuchezewa kwa mita au uharibifu wa mita; na

(e) kupima, kuhifadhi na kubadilisha mita kulingana na mapendekezo ya watengenezaji.

Upimaji na majaribio

38.-(1) Mwenye leseni ya kuzalisha umeme atapima-

(a) uwezo wa kutegemewa wa mitambo

ya kuzalisha umeme na kufanya majaribio ya uendeshaji kwa kufuata masharti ya mkataba wa ununuzi umeme; na

(b) mitambo ya kuzalisha umeme, iwapo kuna ongezeko la uwezo au majaribio ya mitambo mipya ya kuzalisha umeme au mitambo ya kuzalisha umeme ulioboreshwa.

(2) Mwenye leseni ya kuzalisha umeme, ndani ya siku thelathini za
kufanya kazi baada ya kufanya upimaji kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) , atawasilisha kwenye Mamlaka ripoti kuhusiana na hayo.

(3) Mwenye leseni ya uzalisahaji atairuhusu Mamlaka kushuhudia upimaji unaofanyika kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) hapo.

## Sehemu Ndogo ya Pili
### *Wajibu wa Kitaalam wa Mwenye Leseni ya Kupeleka Umeme*

Ruhusa na ofa ya kujiunga au Kutoa huduma ya upelekaji umeme

39.-(1) Mwenye leseni ya kupeleka umeme atafanya yafuatayo: kuruhusu matumizi ya mtandao wa kupeleka umeme kwa watu wenye ujuzi kufuata misingi ya usawa pasipo upendeleo:

(a) kutoa huduma za kupeleka umeme ili kuruhusu kuungiwa huduma, kukatiwa na kurudishiwa huduma kwenda au kutoka kwenye mtandao wake wa upelekaji umeme kwa kufuata masharti ya mfumo husika wa upelekaji umeme, mkataba wa kuunganisha wateja na kanuni na vigezo vinavyotolewa na Mamlaka;

(b) kutoa na kuruhusu mtandao wake wa upelekaji wa umeme kutumiwa kufuata misingi ya usawa pasipo upendeleo kwa mtu yeyote ambaye ataingia mkataba wa jinsi ya kujiunga na mfumo wa upelekaji

umeme au mkataba wa matumizi wa mfumo wa upelekaji umeme.

(c) baada ya kupokea ombi la kujiunga kwenye mtandao wake wa upelekaji umeme atafanya tathmini ya ombi kwa kufuata kanuni, miongozo, maagizo na maelekezo ya Mamlaka;

(d) kuufanya mkataba wa kujiunga na mtandao wa upelekaji umeme na mkataba wa kutumia mtandao wa upelekaji umeme kama mikataba tofauti na pia iwe tofauti na mkataba wowote mwingine wa mauzo ya umeme;

(e) bila kujali ujumla wa aya (f), kumpa mteja yeyote fursa ya kujiunga kwenye mtandao wa upelekaji umeme iwapo kuna uwezo wa kutosha kwenye mtandao wenyewe;

(f) si zaidi ya siku thelathin za kufanya kazi baada ya kufahamishwa juu ya kukubaliwa kwa ofa iliyotolewa chini ya kanuni ndogo (f);

(i) kukamilisha mkataba wa matumizi ya mtandao wa upelekaji umeme na mtu husika; na

(ii) kumuunganisha mtu huyo.

(g) bila kujali masharti ya aya (f), (g) na (h) na baada ya kupokea maombi ya maandishi, kutoa ofa ya kutoa huduma zinazoombwa ndani ya muda muafaka kuzingatia ugumu wa huduma zilizoombwa na vigezo bora vya utendaji kazi; na

(h) kufanya shughuli zote zinazohitajika ili kuruhusu kuunganishwa, kuondoa, na kuunganisha tena huduma kwenye mtandao au kutoka kwenye mtandao wa upelekaji umeme.

Wajibu wa jumla wa mwenye leseni ya upelekaji umeme

40. Mwenye leseni ya upelekaji umeme atafanya-

(a) kusimamia, kuhifadhi na kuendesha mtandao wa upelekaji umeme kuhakikisha kuwa chini ya hali ya kawaida umeme unaendelea kupelekwa kwenye sehemu ya kuingio kwa kufuata:
   (i) michoro ya kitaalam inayohusika; na
   (ii) malengo ya uhakika na ubora wa huduma yaliyoidhinishwa na Mamlaka.

(b) kupunguza idadi ya kuingiliwa kwa huduma au kupungua kwa uwezo kwenye sehemu ya kiungio kwa kufuata vigezo bora na vya busara vya utoaji huduma; na

(c) kurejesha uwezo uliopimwa mapema iwezekanavyo kufuatia kuingiliwa kwa huduma ama:
   (i) kwenye sehemu ya kiungio kwenye mtandao wa upelekaji umeme; au
   (ii) kuhusisha mtandao wa upelekaji umeme.

Haki za mwenye leseni ya upelekaji umeme

41. Mwenye leseni ya upelekaji umeme umeme atakuwa na haki ya:

(a) kuondoa vifaa vinavyomilikiwa na mtumiaji wa mfumo wa usambazaji ambaye anaathiri ukamilifu na usalama wa mtandao wa upelekaji umeme;

(b) kuingia kwenye mfumo unaoendeshwa na mtoa huduma wa soko la

umeme pasipo upendeleo;

(c) kufanya kazi na mwendeshaji wa mfumo wa soko la umeme ili-

(i) kushughulika na ukataji umeme;

(ii) kuwakilisha ubora na uwezo wa mitambo yake; na

(iii) kuamua juu ya athari zinazohusiana na ukataji umeme kwa mitambo yake.

(d) kuweza kupata ripoti, taarifa zisizo za siri na kuingia kwenye tovuti ya mwendeshaji wa mfumo wa soko la umeme; na

(e) ikitokea kuwa mfumo na mwendeshaji wa soko la umeme au mtumiaji wa upelekaji umeme anashindwa kufuata kanuni, atawajibika kuwasilisha malalamiko kwa:

(i) mwendeshaji wa mfumo wa soko la umeme; au

(ii) kwenye Mamlaka.

Ripoti ya utendaji kazi wa mtandao wa upelekaji umeme

42. Mwenye leseni ya upelekaji umeme atawasilisha kwenye Mamlaka ripoti ya kina kuhusu uendeshaji wa mtandao wa upelekeji umeme, ikiwa ni pamoja na uwezo wake, ukataji wa umeme, upotevu wa umeme, ufanisi na uhakika wa mtandao kama itakavyohitajika na Mamlaka.

Kupanga mtandao wa upelekaji umeme na upatikanaji wa ardhi

43. -(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atatayarisha mpango wa kupanua mali na kuendeleza mtandao wa upelekaji umeme.

(2) Mwenye leseni ya upelekaji umeme, si chini ya siku sitini kabla ya kuanza mwaka, kuwasilisha mpango uliotajwa kwenye kanuni ndogo (1) kwenye Mamlaka ili kuidhinishwa.

(3) Mpango ulioelezewa kwenye kannuni ndogo ya (1) utatekelezwa kwa kufuata mpango kazi maalum uliotayarishwa wa kuboresha mtandao wa upelekaji umeme kufikia kiwango kinachokubalika kitaalam na kiuchumi, ukizingatia vigezo vya afya, usalama na mazingira-

(a) ukuaji wa mzigo wa umeme; na
(b) upatikanaji na uhakika wa huduma za upelekaji umeme kwa wateja.

(4) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atawasilisha maombi kwa Mamlaka zinazohusika ili kupata haki ya njia ya umeme juu ya ardhi husika na hivyo kuweza kufikia, kujenga, kuhifadhi au kupanua mtandao wa upelekaji umeme.

(5) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atachukua hatua stahiki katika nyakati tofauti kuhifadhi uhitaji wa ardhi iliyopatikana chini ya kanuni ndogo ya (4).

Mpango wa Kupanua mtandao wa upelekaji umeme

44.-(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atawasilisha kwenye Mamlaka kwa ajili ya uchunguzi mpango wa kupanua mtandao wa upelekaji umeme ambao utakuwa na pendekezo lenye takwimu za kuunga mkono, kupanua au kuboresha mtandao wa upelekaji umeme.

(2) Mpango wa kupanua mtandao wa upelekaji umeme utazingatia yafuatayo:

(a) sera ya Taifa ya nishati;
(b) kukidhi matakwa ya kitaalam, mazingira na kiuchumi;
(c) kuzingatia:
   (i) mahitaji ya umeme kama yanavyobainishwa na mwendeshaji wa mfumo wa soko la umeme;
   (ii) mahitaji ya wateja wapya wanaotaka kujiunga;
   (iii) vigezo vilivyoidhinishwa vya uhakika wa huduma na ubora wa

huduma;

(iv) Mpango wa Muda Mrefu wa Kuendeleza Umeme; na

(v) maombi yoyote ya upanuzi wa huduma kutoka kwa watumiaji wa huduma ya upelekaji umeme au waombaji wa matumizi ya huduma ya kupeleka umeme.

Kipengele cha nguvu ya umeme

45. Mwenye leseni ili kuhakikisha mtandao wa upelekaji umeme unafikia kiwango cha nguvu ya umeme inayotakiwa atafanya yafuatayo:

(a) atafunga vifaa na mitambo ambavyo vinawiana na utendaji bora katika sekta ndogo ya umeme; na

(b) kuhakikisha kuwa mikataba ya kusambaza umeme iliyoingiwa na mwenye leseni inaelezea kwa uwazi wajibu wa mhusika mwingine kwa kufunga vifaa vya kuboresha nguvu ya umem katika sehemu za viungio ambako umeme unapelekwa.

Upotevu wa Umeme Kutokana na upelekaji wa umeme

46.-(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atapunguza upotevu wa umeme katika mtandao wa upelekaji umeme kufikia viwango vilivyoidhinishwa na Mamlaka.

(2) Mwenye leseni atawasilisha kwenye Mamlaka-

(a) ndani ya siku thelathini za mwaka unaofuata, taarifa ya upotevu wa umeme kwenye mtandao wake katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, pamoja na mpango wa kupunguza upotevu huo; na

(b) ndani ya siku thelathini za robo mwaka unaofuata, ripoti ya robo mwaka ya upotevu wa umeme, pamoja na mipango ya mwenye leseni kupunguza upotevu huo.

(3) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atatekeleza masharti na malengo yatakayotolewa na

Mamlaka kuhusiana na mpango wa kupunguza upotevu wa umeme.

Kutii maagizo kutoka kwa mwendeshaji wa soko la umeme

47. Mwenye leseni ya upelekaji umeme kwa wakati wote atafuata maelekezo ya mwendeshaji wa mfumo wa umeme na mwendeshaji wa soko la umeme.

Kuwasilisha taarifa kwa mwendeshaji wa Mfumo na soko la umemm

48. (1) Taarifa inayoelezewa katika kanuni ndogo ya (1) inaweza kuwa nyongeza kwa taarifa ambayo inatakiwa kutolewa chini ya kanuni za soko au chini ya leseni.

(a) endapo kutatokea mabadiliko ya taarifa zilizotajwa kwenye kanuni ndogo (5)(c), kumfahamisha mwendeshaji wa mfumo na soko la umeme ndani ya siku saba za kufanya kazi tokea tarehe ya mabadiliko.

(3) Mwenye leseni hatakiwi kununua au kuuza umeme, isipokuwa:

(a) kufidia hasara kwenye mtandao wa upelekaji umeme ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa vituo vya transfoma; au

(b) kama mteja wa mifumo mingine, kukidhi mahitaji ya utawala.

(4) Mwenye leseni ya upelekaji umeme, ikiwa vifaa vya mtumiaji mfumo wa upelekaji umeme vitashindwa kukidhi mahitaji ya kitaalam na malengo yaliyowekwa, atachunguza na kutoa taarifa kuhusu kushindwa huko kwa Mamlaka au mwendeshaji wa mfumo wa soko la umeme ndani ya siku tatu.

(5) Mwenye leseni ya upekelaji umeme atafanya yafuatayo:

(a) kupokea, kukubali na kutekeleza maagizo yanayotolewa na mwendeshaji wa mfumo na soko la umeme, isipokuwa kwa kufanya hivyo kutaathiri mitambo ya mwenye

leseni au wafanyakazi.

(b) kumfahamisha mwendeshaji wa mfumo wa soko la umeme yafuatayo:

(i) mabadiliko yoyote kwenye vifaa vya upekelaji umeme; au

(ii) vikwazo alivyokumbana navyo mwenye leseni kutokana na Mpango wa Upanuzi wa Mfumo wa Upelekaji Umeme au utaratibu wa kazi na upelekaji umeme.

(c) kuwasilisha kwa mwendeshaji wa mfumo na soko la umeme taarifa zinazotakiwa chini ya-

(i) Sheria;

(ii) Kanuni hizi;

(iii) leseni; na

(iv) kanuni za soko.

Matayarisho kukabili dharura

49.-(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atachukua hatua stahiki kama itakavyotakiwa:

(a) kujitayarisha kwa matukio ya dharura;

(b) kurekebisha mtandao wa upekelaji umeme baada ya ajali; na

(c) kushiriki katika mazoezi na vipimo.

(2) Mwenye leseni ya upelekaji umeme ataweka utaratibu kuhakikisha usalama na uendeshaji endelevu wa mfumo wa umeme wakati wa matukio ya dharura kwa kuzingatia masharti husika ndani ya kanuni za soko na vigezo na kanuni na malengo mengine yanayohusika ambayo yamewekwa au kuidhinishwa na Mamlaka.

Matengenezo ya kawaida

50. -(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atafanya yafuatayo:

(a) atafanya matengenezo ya kinga ya mitambo mara kwa mara kuhakikisha utoaji huduma za upelekaji umeme ni endelevu na za uhakika;

(b) kufanya matengenezo ya kinga ya mara kwa mara kwenye mtandao wake wa upelekaji umeme kwa kufuata kanuni, maelekezo na ratibu zilizoidhinishwa na Mamlaka;

(c) kufanya matengenezo ya dharura au matengenezo makubwa kwenye vifaa vya mtandao wa upelekaji umeme kuhakikisha kuduma endelevu na za uhakika za kupeleka nguvu za umeme; na

(d) kwa kufuata mipango ya matengenezo na uwekezaji iliyoidhinishwa na Mamlaka, kubadilisha na kukarabati vifaa vya mtandao ambavyo:

(i) muda wa matumizi unakaribia kumalizika; au

(ii) vimeharibika pasipo sababu.

(2) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atapanga na kutoa mpango wa mwaka na wa muda mrefu wa shughuli za matengenezo kwa kumshirikisha mwendeshaji wa mfumo na soko la umeme.

(3) Mpango wa matengenezo na utaratibu ulioelezwa kwenye kanuni ndogo (2) utapangwa kwa kuzingatia:

(a) kanuni au miongozo inayotolewa na Mamlaka; na

(b) kupunguza jumla ya gharama za umeme uliopelekwa na kwa wakati huo kuhifadhi uhakika wa mtandao wa upelekaji umeme.

Mwenye leseni ya upelekaji umeme

51. –(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atafanya yafuatayo:

(a) endapo mtambo na vifaa vilivyoharibiwa vitasababisha hali ya hatari au uwezekano wa watu kuumia au uharibifu wa mali, mara moja baaada ya kufahamishwa kuhusu uharibifu, kuondoa hali hiyo ya hatari

kabla ya kufanya matengenezo ya dharura au ukarabati;

(b) kwa haraka kufanya matengenezo ya vifaa vilivyoharibika vya mtandao wa upelekaji umeme na kisha kuwaunganisha tena washiriki wa soko la umeme mapema iwezekanavyo; na

(c) kufanya shughuli za kubadilisha vifaa na kufanya ukarabati unaotakiwa kwa kufuata mipango ya ukarabati na uwekezaji iliyopata idhini ya Mamlaka.

Matengenezo ya kinga ya mitambo

53. Mwenye leseni ya upelekaji umeme atahakikisha kuwa kukatisha kwa huduma ya upelekaji umeme unaotegemewa kutokea unapangwa kudumu kwa kipindi kifupi kama itakavyowezekana.

Kukatisha huduma

54. Mwenye leseni ya upelekaji umeme atatoa taarifa kwa Mamlaka kwa maandishi endapo kutatokea ukataji wa huduma kwa ajili ya matengenezo ya dharura, ukarabati au matengenezo ya kukinga mitambo ambayo yanaathiri huduma za upelekaji umeme kwa zaidi ya siku mbili mfululizo.

Kukatika kwa umeme

55. Mwenye leseni ya upelekaji umeme, kwa kushauriana na mweneshaji wa mfumo na soko la umeme, anaweza kujikomboa kutoka kwenye ukataji umeme unaotokea kwenye mtandao wa upelekaji umeme na kuanza kutoa huduma za upelekaji umemem mapema iwezekanavyo.

Notisi ya kukata huduma

56.-(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme, pale anapotaka kufanya matengenezo ya kinga, kubadilisha vifaa, kuboresha huduma au kufanya ujenzi wowote ambao utasababisha kuwa na katizo la huduma au kupunguza huduma za kupeleka umeme, kutoa notisi kwa umma kuhusu hilo, si chini ya siku tatu za kazi kabla ya kutekeleza shughuli hizo.

(2) Notisi inayoelezwa kwenye kanuni ndogo ya(1) itakuwa ni pamoja na tarehe na saa ya katizo la huduma ya upelekaji umeme na tarehe na saa ya kurudisha huduma.

Mita

57.-(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atafunga, atahifadhi, na kuthibisha usahihi wa ufungaji mita za umeme katika sehemu zote za kuchukulia umeme kutoka kwenye mtandao wa upelekaji umeme.

(2) Mwenye leseni ya upelekaji umeme, kuhusu ufungaji wa mita ulioelezwa kwenye kanuni ndogo ya (1), atafuata vigezo vya ufungaji mita na kanuni zilizotayarishwa na Mamlaka.

(3) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atawasilisha kwa washiriki wa soko la umeme takwimu zote zinazotakiwa katika kukokotoa mafanikio ya wajibu wa pande zinazohusika, au kutatua mzozo wowote unaohusiana na mikataba baina ya nchi husika.

(4) Mwenye leseni ya upelekaji umeme atakadiria kiwango cha umeme unaotumika wakati wa kipindi ambacho mita imesimamishwa kufanya kazi au ina hitilafu kwa kufuata kanuni za soko.

Mpango wa Kuboresha Utendaji

58. -(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme, ndani ya mwaka mmoja baada ya kupata leseni, atathibitisha misingi yake ya uendeshaji na mpangilio wa kazi, misingi ambayo itatumika kuanzisha mpango wa kuoresha utendaji kazi ambao utapata idhini ya Mamlaka.

(2) Mpango unaotakiwa chini ya kanuni ndogo ya (1) utakuwa na-

(a) malengo maalum ya kuboresha huduma kwa kutengeneza viashiria muhimu vya utendaji kazi na kuanzisha mbinu za kutathmini mafanikio; na

(b) kama lazima zitatengenezwa kwa kufuata kanuni au maelekezo ya Mamlaka.

(3) Mwenye leseni ya upelekaji umeme, kwa

kila mwaka anatakiwa kutathmini na kuwasilisha kwa Mamlaka mpango ulioelezwa kwenye kanuni ndogo (1) ili upate idhini ya Mamlaka.

Mpango wa kuhakiki ubora

59. -(1) Mwenye leseni ya upelekaji umeme ataanzisha mpango ambao utahakiki kwa kina ubora wa kutoa huduma za upelekaji umeme, na kufanya marekebisho stahiki kwa kufuata maagizo ya Mamlaka.

(2) Mwenye leseni ya upelekaji umemem, si chini ya siku tisini (90) baada ya kupata leseni, atatakiwa kuwasilisha mpango wa kuthibitisha ubora wa huduma kwa Mamlaka ili kupata idhini yao.

## Sehemu Ndgo ya Tatu
## Wajibu wa Kitaalam wa Mwenye Leseni ya Usambazaji Umeme

Huduma za Usambazaji Umeme

59. -(1) Mwenye leseni ya usambazji umeme atafanya yafuatayo:

(a) kutoa huduma ya usambazaji umeme kwa wateja kwa misingi ya usawa pasipo upendeleo.

(b) kufanya shughuli zote zinazotakiwa kuruhusu kuungiwa huduma, kukatiwa, na kurudishiwa huduma kwenda au kutoka kwenye mtandao wa usambazaji umeme kwa kufuata kanuni za usambazaji, na vigezo vingine vinavyotolewa au vilivyoidhinishwa na Mamlaka; na

(c) kutopunguza au kusitisha huduma za usambazaji umeme kwa mteja isipokuwa kama mteja ameshindwa kulipia huduma au tozo ndani ya kipindi husika au ameshindwa kutii masharti ya mkataba wa usambazaji umeme.

Mkataba wa usambazaji umeme

60. -(1) Mwenye leseni ya usambazaji umeme atakamilisha mikataba ya usambazaji umeme na kila mteja.

(2)Mwenye leseni ya usambazaji umeme atahakikisha kuwa mkataba wa usambazaji umeme angalau una taarifa zifuatazo:

(a) wadhifa wa mwenye leseni na anuani yake;

(b) ukubwa wa huduma zitakazotolewa;

(c) aina ya matengenezo na huduma mteja atakayopatiwa;

(d) utaratibu utakaotumika kumpatia taarifa mteja kuhusu bei na tozo nyingine;

(e) ukomo wa mkataba;

(f) masharti ya kuomba tena au kusitisha mkataba; na

(g) uwepo wa fidia au mipango ya kurudisha malipo endapo malengo ya ubora wa huduma yaliyokubaliwa hayatafikiwa.

Mpango wa mtandao wa Uuambazaji na upatikanaji wa ardhi

61. -(1) Mwenye leseni ya usambazaji umeme, kwa kufuata kanuni zilizotolewa na Mamlaka anatakiwa kutayarisha mpango wa kupanua mali na maendeleo ya mtandao wa usambazaji umeme.

(2) Mwenye leseni ya usambazaji umeme, si chini ya miezi miwili kabla ya mwaka kuanza, kuwasilisha mpango uliotajwa kwenye kanuni ndogo ya (1) kwenye Mamlaka ili kuidhinishwa.

(3) Mpango ulioelezwa kwenye kanuni ndogo (1) utatekelezwa kwa kufuata mpango kazi maalum uliotengenezwa wa kuboresha mtandao wa usambazaji umeme kufikia kiwango kinachokubalika kiutaalam na kiuchumi, ukizingatia:

(a) vigezo vya afya, usalama na mazingira;

(b) ukuaji wa mzigo wa umeme; na

upatikanaji na uhakika wa huduma za usambazaji umeme.

(4) Mwenye leseni ya usambazaji umeme atawasilisha maombi kwa Mamlaka husika ili kupata haki ya njia ya umeme juu ya ardhi husika na hivyo kuweza kufikia, kujenga, kuhifadhi au kupanua mtandao wa usambazaji umeme.

(5) Mwenye leseni ya usambazaji umeme atachukua hatua stahiki katika nyakati tofauti kuhifadhi uhitaji wa ardhi iliyopatikana chini ya kanuni ndogo ya (4).

Makadirio ya kiasi cha umeme

62. -(1) Mwenye leseni ya usambazaji umeme atawasilisha makadirio ya umeme kila mwaka, na kama itakavyotakiwa na Mamlaka

(2) Mwenye leseni ya usambazaji baada ya kanuni hizi kuanza kufanya kazi atatakiwa kuanza kuwasilisha kwenye Mamlaka ili kupata idhini makadirio ya umeme ndani ya mtandao wa usambazaji umeme, kwa kipindi cha miaka mitatu kufuatana.

(3) Mwenye leseni ya usambazaji umeme atapeleka kwenye Mamlaka;

(a) matumizi halisi ya umeme yaliyofikiwa kutokana na uchunguzi wa kiasi cha umeme uliotumiwa na kila aina ya mteja ambako umeme unapimwa na;

(b) idadi ya wateja na muhtasari wa mahitaji ya umeme kwa kila aina ya mteja.

Ulinzi na usalama wa umeme

63. Mwenye leseni ya usambazaji umeme atawapa wateja wake anuani ya kuwasiliana ambayo itatumiwa na wateja wake kutoa taarifa kwa mwenye leseni kuhusu jambo lolote au tukio linalohusiana na upatikanaji wa huduma za usambazaji umeme ambalo;

(a) litaleta hatari au linahitaji kushughulikiwa haraka; au

(b) linaathiri au litaathiri usalama wa huduma ya umeme, upatikanaji au ubora wa huduma ya usambazaji umeme

Ubora wa huduma

64. –(1) Mwenye leseni ya usambazaji umeme, si chini ya miezi sita baada ya kupokea leseni, atatakiwa kuwasilisha kwenye Mamlaka kwa kuidhinishwa malengo ya ubora wa huduma za usambazaji na ubora wa Malengo ya ubora wa huduma na ubora wa utoaji umeme yaliyoelezwa chini ya kanuni ndogo ya (1) yatazingatia vigezo vya utoaji huduma ulio bora na wenye busara.

(2) Mwenye leseni ya usambazaji umeme si chini ya siku tisini (90) baada ya kupata idhini chini ya kanuni ndogo ya (1) atatakiwa kuwasilisha mpango wa jinsi ya kufikia malengo hayo.

Kipengele cha nguvu za umeme

65. Mwenye leseni ya usambazaji atafunga vifaa na mitambo vinavyotakiwa kuhakikisha kuwa kipengele cha nguvu za umeme kwenye mtandao wa usambazaji umeme kinafikia kiwango kinachotakiwa ikiwa ni pamoja na kufunga vifaa vya kupima ubora kwenye sehemu husika kwenye mtandao.

Upotevu wa umeme kwenye mtandao wa usambazaji

66. -(1) Mwenye leseni ya usambazaji umeme atafanya yafuatayo:

(a) ndani ya mwaka mmoja baada ya kanuni hizi kuanza kutumika, kuwasilisha ripoti inayobainisha kiwango cha upotevu wa umeme kwenye mtandao wa usambazaji umeme pamoja na taarifa ya wateja waliojiunga pasipo kufuata taratibu; na
(b) kupendekeza malengo ya upotevu wa umeme ambayo yanaweza kufikiwa kwenye Mamlaka ili kuidhinishwa

(2) Mwenye leseni ya usambazaji umeme atawasilisha kwenye Mamlaka taarifa ya upotevu wa umeme kwenye mtandao wa usambazaji umeme katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, pamoja na mpango wa kupunguza upotevu huo.

Matayarisho kukabili hali ya dharura

67.-(1) Mwenye leseni ya usambazaji umeme;

(a) atachukua hatua stahiki kama itakavyotakiwa kujitayarisha kwa matukio ya dharura na kurekebisha mtandao wa usambazaji umeme; na

(b) kuanzisha na kutekeleza utaratibu ndani ya viwango vya kitaalam vinavyohusika kuhakikisha usalama na uendeshaji endelevu wa mtandao wa usambazaji umeme wakati wa matukio ya dharura.

Ukataji umeme uliopangwa na matengenezo ya kinga ya mitambo

68. Mwenye leseni ya usambazaji umeme atafanya shughuli za matengenezo ya kukinga mitambo kuhakikisha huduma endelevu na za uhakika za usambazaji umeme.

(2) Mwenye leseni ya usambazaji umeme atatoa taarifa kwa umma kuhusu ukataji wa umeme uliopangwa pamoja na muda utakaotumika si chini ya siku saba kabla ya kutokea tukio lolote la ukataji huduma.

(3) Mwenye leseni ya usambazaji wakati wa kufanya matengenezo ya kukinga mitambo, kubadilisha vifaa, kuboresha huduma au kufanya ujenzi wowote ambao utasababisha kusimamisha huduma za kusambaza umeme kwa zaidi ya saa ishirini na nne.

(a) kutoa taarifa kwenye Mamlaka na kwa umma angalau siku tatu (3) kabla ya kusitisha kwa muda wa huduma ya usambazaji umeme; na

(b) kuhakikisha kuwa ukataji wa huduma zote za usambazaji umeme unaotegewa kutokea unapangwa kudumu kwa kipindi kifupi

Kukata Umeme

69. Mwenye leseni ya usambazaji wa umeme

na matengenezo ya dharura

atafanya yafuatayo:

(a) mara moja kuchukua hatua stahiki kurudisha huduma endapo usambazaji na upatikanaji wa umeme kwenye kiungio kwa mteja kimeingiliwa kwa sababu yoyote ile ikiwa ni pamoja na kukatika kwa umeme kitendo ambacho hakikupangwa;

(b) endapo mtambo na vifaa vilivyo haribiwa vitasababisha hali ya hatari au uwezekano wa watu kuumia au uharibifu wa mali, mara moja baada ya kufahamishwa kuhusu uharibifu huo, kuondoa hali hiyo ya hatari kabla ya kufanya matengenezo ya dharura au ukarabati; na

(c) kwa haraka zaidi kufanya matengenezo ya mtambo na vifaa vilivyoharibika na dosari nyingine za mitambo na kisha kuwaunganishia tena wateja kama itakavyobainishwa kwenye mkataba wa huduma kwa mteja.

Notisi ya kukata huduma ya usambazaji

70. Mwenye leseni ya usambazaji umeme ataifahamisha Mamlaka na wateja kwa maandishi, kama kutakuwa na kuingiliwa kwa huduma ya kusambaza umeme kwa madhumuni ya kusambaza umeme;

(a) ukarabati au matengenezo ya kinga ya mitambo na kama kuingiliwa kwa huduma kutaathiri utoaji wa huduma za usambazaji umeme; na

(b) matengenezo ya dharura,ikiwa kuingiliwa kwa huduma kunaathiri utoaji huduma za usambazaji kwa zaidi ya saa arobaini na nane .

Ufungaji mita

71. -(1) Mwenye leseni atafanya yafuatayo:

(a) kutoka kila sehemu palipofungwa mita, atapeleka kwa mwenye leseni ya uzalishaji umeme, mwenye leseni ya upelekaji umeme au mtu mwingine yeyote takwimu zote zinazotakiwa ili kukokotoa kufikiwa kwa majukumu au kutatua mzozo wowote unaohusika na mkataba;

(b) kufunga, kuhifadhi, na kwa mapendekezo ya mtengenezaji mita, kuthibitisha usahihi wa ufungaji mita za umeme kwenye maeneo yote ya uchukuaji umeme kutoka kwenye mtandao wa usambazaji umeme; na

(c) endapo kutatokea hitilafu au uharibifu wa mita kwa sababu yeyote ile nje ya uwezo wa mteja, kutengeneza hitilafu hiyo au uharibifu au kubadilisha mita mapema iwezekanavyo.

(2) Umeme uliotumika wakati mita imesimamishwa au ina hitilafu utakadiriwa kwa kufuata-

(a) kwa mteja mkubwa, mkataba unaohusika; na

(b) kwa wateja wengine, na kwa kutokuwepo mkataba ukadiriaji utafanywa kwa kutumia mwenendo wa matumizi.

(3) Bila kujali matakwa ya kanuni ndogo (2)(b), endapo mteja hataridhika na kiwango kilicho kadiriwa, atapeleka malalamiko yake kwenye Mamlaka kwa uamuzi na Mamlaka itashughulikia jambo hilo kwa kufuata masharti ya sheria ya Mamlaka ya Udhiiti Nishati na Maji.

Sura 414

Kugundua na kuzuia wizi, uharibifu na kuchezea mita

72. Mwenye leseni ya usambazaji umeme atachukua hatua stahiki kugundua na kuzuia-

(a) wizi wa umeme kwenye eneo la kutoa huduma;

(b) uharibifu au hitilafu kwenye mitambo ya umeme na mita za umeme kwenye eneo la

kutolea huduma;
(c) kuchezea mita za umeme kwenye eneo la huduma; na
(d) matumizi ya umeme yasio na taarifa kwenye eneo la kutolea huduma.

Mpango wa kuboresha utendaji

73. -(1) Mwenye leseni ya usambazaji umeme, ndani ya mwaka mmoja baada ya kanuni hizi kuanza atathibitisha misingi yake ya utendaji na mpangilio wa kazi, misingi ambayo itatumika kuanzisha mpango wa kuboresha utendaji kazi ambao utapata idhini ya Mamlaka ambako misingi iko chini ya malengo yanayotakiwa. Mpango unaotakiwa chini ya kanuni ndogo ya (1) utakuwa na-
(a) malengo maalum ya kuboresha huduma kwa kutayarisha viashiria muhimu vya utendaji kazi na kuanzisha mbinu za kutathimini mafanikio; na
(b) kama lazima, zitayarishwe kwa kufuata kanuni na maelekezo ya Mamlaka.

(2) Mwenye leseni ya usambazaji, kwa kila mwaka, anatakiwa kutathimini na kuwasilisha kwenye Mamlaka mpango ulioelezewa kwenye kanuni ndogo (2) ili upate idhini ya Mamlaka.

## SEHEMU YA SITA
## UTEUZI WA WATEJA MUHIMU

Maombi ya kuwa mteja muhimu

74.-(1) Mtu yeyote mwenye sifa zinazotakiwa na anataka atambuliwe kama mteja muhimu atawasilisha ombi lake kwenye Mamlaka kama inavyoelezewa kwenye Jedwali.

(2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatana na nyaraka zifuatazo:
(a) ushahidi wa uwezo wa kutumia umeme;
(b) mkataba wa upelekaji umeme kama upo; na
(c) barua ya kuthibitisha kutoka kwa msambazaji umeme kuwa mwombaji hana

madeni pale inapomhusu.

Vigezo vya uteuzi wa mteja muhimu

75. –(1) Maombi ya kuteuliwa kama mteja muhimu yanatakiwa yakidhi vigezo vifuatavyo:

(a) mwombaji awe anapata umeme wenye nguvu si chini ya 33kv;

(b) Mwombaji awe na mahitaji ya umeme wa kiwango cha juu cha megawati mbili au zaidi; na

(c) kama mwombaji anapelekewa umeme na mwenye leseni ya usambazaji, anatakiwa kupata barua ya kuthibitisha hayo kutoka kwa mwenye leseni ya usambazaji ili kuihakikishia Mamlaka kuwa hakuna madai yoyote na hadai lolote.

(2) Bila kujali masharti chini ya kanuni ndogo (1),Mamlaka inaweza kukubali ombi la kuwa mteja muhimu pasipo mteja kufikia viwango husika kama hali inaruhusu kufanya hivyo.

Haki za mteja muhimu

77. Mteja yeyote anayepewa wadhifa wa kuwa mteja muhimu na Mamlaka atakuwa na haki zifuatazo;

(a) kununua umeme kutoka kwa mwenye leseni ya kuzalisha umeme anaye mtaka yeye;

(b) kuingia Mkataba wa Ununuzi Umeme na mwenye leseni ya kuzalisha umeme pasipo idhini ya Mamlaka; na

(c) kuingia katika majadiliano ya bei ya umeme kuzingatia uelewano uliopo na muuzaji umeme,

Masharti kuwa na nguvu

77. Masharti ya Sehemu hii yatakuwa na nguvu zaidi juu ya kanuni nyingine zitakazotayarishwa na Mamlaka na ikitokea kutofautiana masharti ya sehemu hii yatatumika

## SEHEMU YA SABA
## UFUATILIAJI NA UTEKELEZAJI

Ukaguzi

78.-(1) Mamlaka baada ya kutoa notisi kwa mwenye leseni, atakagua miundombinu ya mtoa huduma na nyaraka mbalimbali, na mwenye leseni anatakiwa kutoa msaada wowote unaotakiwa wakati wowote wa kufanya ukaguzi wa shughuli inayodhibitiwa. Wakati wa ukaguzi Mamlaka itafanya yafuatayo:

(a) kutoa nakala za nyaraka muhimu pamoja na vitabu, akaunti za fedha au taarifa nyingine zinazowekwa na mwenye leseni chini ya sheria husika;
(b) kukagua mashine, vifaa, mita na vikorombwezo vingine na kuchukua vipimo au kurekodi tarrifa za kitaalam ikiwa ni pamoja na matumizi ya umeme, viwango vya nguvu ya umeme, masafa ya umeme, upatikanaji wa umeme na utekelezaji wa mkataba wa huduma kwa mteja; na
(c) kuingia kwenye mifumo ya programu ya kompyuta ya mwenye leseni kama itaonekana ni lazima.

Wajibu wa Mamlaka wakati wa ukaguzi

79. –(1) Wakati wa ukaguzi, ofisa au mwakilishi wa Mamlaka atatakiwa kufanya yafuatayo:

(a) kueleza wadhifa wake kwa mwenye leseni au mteja kwa kutumia kitambulisho kilichotolewa na Mamlaka;
(b) kumwelezea mwenye leseni au mteja madhumuni ya kufanya ukaguzi;
(c) kufanya kazi kwa usawa, malengo na uadilifu;
(d) kutojishughulisha na mambo ya kibaguzi, upendeleo au kunyanyasa;
(e) kujiepusha na migongano ya kimaslahi;
(f) kufanya ukaguzi kwa kutumia ujuzi na utaalam kulingana na mahitaji ya kanuni hizi, vigezo, malengo, miongozo, orodha ya

ukaguzi, sheria husika na vigezo vya ubora na busara; na

(g) kutotumia nguvu au lugha inayotishia na ya matusi kwa mwenye leseni.

(2) Mtu ambae hataridhika na tendo la afisa au mwakilishi wa Mamlaka wakati wa ukaguzi anaweza, ndani ya siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya kutokea tendo, kutoa taarifa kwa maandishi kwenye Mamlaka.

(3) Baada ya kupokea malalamiko chini ya kanuni ndogo (2) Mamlaka itachunguza malalamiko na kutoa uamuzi kulingana na utaratibu uliopo ndani ya Mamlaka.

Vitendo vinavyokatazwa

80. Mwenye leseni hatakiwi kufanya yafuatayo:

(a) kumzuia au kumkataza afisa au mwakilishi wa Mamlaka kutenda kazi za ukaguzi zinazoruhusiwa chini ya Kanuni hizi au sheria;

(b) kutumia lugha chafu, inayotishia au ya matusi;

(c) kukataa au kushindwa kutii maagizo halali, maelekezo au notisi; na

(d) anapotakiwa kujibu swali anakataa au anashindwa kujibu swali hilo kulingana na ufahamu na utaalam alionao mwenye leseni.

## SEHEMU YA VIII
## MENEJIMENTI YA CHUMBA CHA UDHIBITI

Mahitaji ya Jumla

81 Mwenye leseni kwa wakati wote anatakiwa kuzingatia mahitaji ya jumla yafuatayo wakati wa kuendesha chumba cha udhibiti:

(a) kuwa na angalau mdhibiti mmoja wa chumba cha udhibiti kwa kila chumba;

(b) kuwa na utaratibu wa kimaandishi utakao waongoza waendeshaji wa vyumba vya udhibiti;

(c) kuwa na utaratibu wa uendeshaji uliounganishwa na mipango ya kushughulikia dharura;

(d) muundo wa chumba cha udhibiti kinachotakiwa kiwe na uwezo wa kuhimili majanga au matukio makubwa ya hatari;

(e) mpangilio wa chumba cha udhibiti, na mpangilio wa paneli na kitengo cha kuonyesha picha, viwe katika hali ambayo inawezesha ufanisi na uendeshaji wa uhakika wa mitambo wakati wa hali ya kawaida na hali ya dharura; na

(f) chumba cha udhibiti wakati wote kiwe kinafanya kazi.

Wajibu

82. Mwenye leseni wakati wowote-

(a) anatakiwa kufuata taratibu za kijimenejimenti (kiutawala) za chumba cha udhibiti zilizo chapishwa ambazo zinakidhi masharti ya kanuni hizi;

(b) kuwa na chumba cha udhibiti ambacho kimetengenezwa kuhakikisha kuwa hatari zozote zile zitakazo wakabili wafanyakazi wa chumba cha udhibiti zinakuwa ndani ya viwango vinavyo kubalika;

(c) kuwa na chumba cha udhibiti ambacho kinakidhi madhumuni ya kudhibiti mitambo ya umeme;

(d) kuwa na chumba cha udhibiti ambacho kina mpango wa dharura wa kufuata wakati wa kushughulikia vitendo vya dharura visivyotegemewa kutokea, ndani ya miundombinu ya umeme;

(e) kuajiri watu wenye ujuzi na ufahamu kuendesha chumba cha udhibiti wa umeme;

(f) kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti ili waweze kutekeleza wajibu na majukumu yao

kama yanavyo bainishwa na mwenye leseni; na

(g) kutengeneza na kuhifadhi mwongozo wa uendeshaji na matengenezo ya vifaa.

Taratibu

83. –(1) Kila mwenye leseni atatayarisha na kufuata mwongozo wa utaratibu uliochapishwa wa kufanya uendeshaji, matengenezo na uendeshaji wa dharura.

(2) Mwongozo utakuwa na yafuatayo:

(i) utaratibu wa usalama utakaofuatwa wakati wa kufanya matengenezo na uendeshaji wa kawaida; na

(ii) utaratibu wa kushughulikia uendeshaji usio wa kawaida.

(3) Mwongozo utafanyiwa uhakiki na kuboreshwa na mwenye leseni angalau mara moja kila mwaka.

(4) Mwongozo wa awali utahifadhiwa na watu husika;

(5) Nakala ya mwongozo utawekwa kwenye maeneo ambako shughuli za uendeshaji na matengenezo zitafanyika.

Kuzingatia utaratibu wa dharura

84. Mwenye leseni anatakiwa kufahamu vizuri utaratibu wa kushughulikia dharura na anatakiwa wakati wote kufuata mpango wake ulioidhinishwa wa kuhudumia matukio ya dharura.

(2) Mwenye leseni atajumuisha mafunzo yaliyopatikana, ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa matukio yote yaliyotolewa taarifa, au ajali, kwenye Menejimenti ya Chumba cha Udhibiti, na atahifadhi nyaraka kuonyesha kuwa kwenda tofauti na utaratibu uliowekwa ulikuwa sahihi kwa uendeshaji salama wa vifaa vya umeme.

(3) Mwenye leseni atahakikisha kuwa

mabadiliko ya muonekano wa miundombinu ya umeme na upangaji wa shughuli unaratibiwa kati ya wawakilishi wa chumba cha udhibiti, uratibu wa uendeshaji na watumishi walio nje ya chumba cha udhibiti, wote hawa wanajumuika pamoja wakati wa dharura.

(4) Mwenye leseni atafanya-

(a) atatoa mafunzo husika kwa waendeshaji kuhakikisha kuwa wana uelewa wa utaratibu wa kushughulikia matukio ya dharura; na

(b) kuchunguza shughuli za wafanyakazi ili kujua kama taratibu zinafuatwa katika tukio la dharura.

(5) Mwenye leseni ataanzisha na kuhifadhi mawasiliano na vyombo husika vya moto, polisi na maofisa wengine ili-

(a) kuelewa wajibu na rasilimali za kila chombo kinachoshughulikia dharura ikitokea;

(b) kujifahamisha na vyombo husika vya kushughulikia dharura kujua uwezo wao wakati wa dharura;

(c) kubaini aina za dharura ambazo zinaweza kutolewa taarifa kwa vyombo husika vingine; na

(d) kupanga jinsi mwenye leseni na chombo kingine kinachohusika na masuala ya dharura wanaweza kushirikiana kupunguza ajali kwa maisha au mali.

Wajibu na majukumu

85. –(1) Kila mwenye leseni anatakiwa kujua wajibu na majukumu ya uendeshaji wa chumba cha udhibiti wakati wa hali ya kawaida na isiyo ya kawaida, na mazingira ya uendeshaji wakati wa dharura.

(2) Ili kuhakikisha kuwa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti anachukua hatua stahiki kwa haraka kulingana na mazingira ya uendeshaji, mwenye leseni atafafanua kila jambo kama ifuatavyo;

(a) mamlaka na wajibu wa mwendeshaji wa

chumba cha udhibiti kufanya maamuzi na kuchukua hatua wakati wa uendeshaji wa kawaida;

(b) wajibu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti wakati dharura isiyo ya kawaida inapogundulika, hata kama mwendeshaji sie mtu wa kwanza kugundua hali hiyo, pamoja na jukumu la mwendeshaji wa chumba cha udhibiti kuchukua hatua maalum za kushughulikia tatizo na kuwasiliana na wengine wanaohusika;

(c) wajibu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti wakati wa dharura, hata kama yeye sie mtu wa kwanza kugundua tatizo, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua maalum na kuwasiliana na wengine;

(d) njia ya kuweka kumbukumbu za mwendeshaji wa chumba cha udhibiti kuhusu mabadiliko ya saa za kazi na kupokezana majukumu ya kazi kati ya waendeshaji wa chumba cha udhibiti au kutayarisha mfumo wa kuweka taarifa wakati mwendeshaji ana jukumu la kufuatilia au kudhibiti sehemu yeyote ya miundombinu ya umeme;

(e) wajibu, majukumu na nyadhifa za wengine wenye mamlaka ya kuelekeza au kwenda juu ya hatua maalum za kitaalam ambazo mwendeshaji wa chumba cha udhibiti angechukua;

(f) kuanzisha muda wa kufanya kazi kwa awamu, utaratibu wa kupokezana na kuanzisha kiwango cha juu cha saa za kutoa huduma ili kuhakikisha kuwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti wanaweza kupata saa nane za kulala wakati wa hali ya kawaida ya uendeshaji; na

(g) kutoa elimu na mafunzo kwa wafanya kazi

wanaohusika juu ya uchovu na jinsi ya kuhimili uchovu.

Taarifa Inayotosheleza

86. –(1) Kila mwenye leseni anatakiwa kuwapatia waendeshaji wa chumba cha udhibiti taarifa, vifaa, taratibu na utaratibu ambao ni muhimu kwa waendeshaji kutekeleza wajibu na majukumu yao.

(2) Mwenye leseni atafafanua utaratibu kwa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti ili kumwezesha kutekeleza yafuatayo:

(a) kufanya tathimini ya kila sehemu kati ya picha za SCADA na vifaa husika nje ya chumba wakati vifaa hivyo vimejumuishwa au kuondolewa na wakati mabadiliko mengine yanayoathiri usalama wa miundombinu ya umeme yanafanywa kwa vifaa au picha za SCADA;

(b) kupima na kuthibitisha mpango wa ndani wa mawasiliano ili kutoa nyenzo za kutosha za kuendesha kwa kutumia mikono na kwa usalama, miundombinu ya umeme;

(c) kupima mfumo dada wa SCADA angalau mara moja kwa mwaka; na

(d) kuanzisha na kutekeleza utaratibu wa kumwezesha mwendeshaji tofauti wa chumba cha udhibiti kutekeleza majukumu yake, ikiwa ni pamoja na aina ya taarifa ya kubadilishana.

Kuhimili uchovu

87. Mwenye leseni atatekeleza mbinu zifuatazo ili kupunguza ajali zinazotokana na uchovu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti ambao unaweza

kupunguza uwezo wake wa kutekeleza wajibu na majukumu yake:

(a) kuanzisha muda wa kufanya kazi kwa awamu na utaratibu wa kupokezana ambao utawezesha kupata muda wa kutokufanya kazi unaoruhusu angalau saa 8 za kulala;

(b) kutoa elimu kwa waendeshaji na wasimamizi ya jinsi ya kushughulikia uchovu na jinsi kazi za ziada zinavyoweza kuongeza uchovu.

(c) kutoa elimu kwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti na wasimamizi ili watambue athari za uchovu; na

(d) kuanzisha kiwango cha juu cha saa za kazi kwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti, ambacho kitaruhusu pia wakati wa dharura kuchepuka kutoka kwenye kiwango cha juu kama ni lazima, kwa uendeshaji usalama wa miundombinu ya umeme.

Menejimenti ya onyo la hatari

88. – (1) Kila mwenye leseni anayetumia mfumo wa SCADA atakuwa na mpango ulioandikwa wa kushughulikia onyo la hatari ili mwendeshaji wa chumba cha udhibiti aweze kushughulikia kwa uhakika onyo la hatari.

(2)Mpango wa mwenye leseni utakuwa na masharti ya-

(a) kuhakiki uendeshaji wa vifaa vya onyo la hatari vya SCADA kwa kutumia mfumo ambao unahakikisha vifaa hivyo viko sahihi na vina sababisha usalama katika shughuli za uendeshaji;

(b) kubaini angalau mara moja kwa mwezi sehemu zinazoathiri usalama ambazo zimeondolewa katika kuchunguzwa ndani ya mfumo wa SCADA, zimezuia vifaa vya onyo kutofanya kazi vizuri, zimesababisha kelele za onyo zisizo na ukweli, au zimelazimisha matumizi ya mikono kwa saa

nyingi zaidi ya zile zinazotakiwa katika kufanya matengenezo yanayotakiwa, au kufanya shughuli za uendeshaji.

(c) kuthibitisha usahihi wa thamani ya vifaa vya kutoa onyo la hatari na maelezo ya vifaa hivyo angalau mara moja kwa mwaka;

(d) kuhakiki mpango wa kushughulikia knyo la hatari unaotakiwa chini ya kanuni hii angalau mara moja kwa mwaka kubaini ufanisi wa mpango;

(e) kila mwaka, mwenye leseni atafanya yafuatayo:

(i) kupima na kuthibitisha mpango wa ndani wa mawasiliano kwa uendeshaji wa miundombinu ya umeme kwa kutumia mikono; na

(ii) kupima mifumo Dada ya mifumo ya SCADA.

Kuthibitisha SCADA

89. (1) Mwenye leseni atafanya tathimini ya kila sehemu kati ya picha za SCADA na vifaa husika nje ya chumba wakati vifaa hivyo vimejumuishwa au kuondolewa na wakati mabadiliko mengine yanayo athiri usalama wa miundombinu ya umeme yanafanywa kwa vifaa au picha za SCADA.

(2) Mwenye leseni ataamua kuhusu mabadiliko ambayo yanaathiri usalama wa miundombinu ya umeme, na kufanya uhakiki kama inavyotakiwa kwa maboresho ya mfumo hapo baadaye.

Mabadiliko ya usimamizi

90. Mwenye leseni atahakikisha kuwa mabadiliko ambayo yanaweza kuathiri uendeshaji wa chumba cha udhibiti yanaratibiwa pamoja na wafanyakazi wa chumba cha udhibiti kwa kufanya kila jambo kama ifuatavyo:

(a) kuanzisha mawasiliano kati ya wawakilishi wa chumba cha udhibiti; utawala na

wafanyakazi wa nje wanaohusika wakati wa kupanga na kutekeleza mabadiliko ya muonekano wa miundombinu ya umeme au "kuratibu namna ya kupanga";

(b) kuwataka wafanyakazi wa nje kuwasiliana na chumba cha udhibiti wakati hali ya dharura inapotokea na wakati wa kufanya mabadiliko kwenye maeneo ambayo yanaathiri uendeshaji wa chumba cha udhibiti; na

(c) kushirikisha chumba cha udhibiti au menejimenti ya chumba cha udhibiti kushiriki katika kupanga kabla ya kutekeleza mabadiliko makubwa ya namna ya kupanga.

Uzoefu wa uendeshaji

91. Mwenye leseni atahakikisha kuwa mafunzo yaliyopatikana kutokana na uzoefu wake wa kuendesha shughuli yanajumuishwa, kama inavyotakiwa, kwenye utaratibu wa kuendesha chumba cha udhibiti kwa kufanya yafuatayo:

(a) Mwenye leseni atachunguza matukio yanayotolewa taarifa ili kubaini kama hatua zinazo chukuliwa na chumba cha udhibiti zimechangia kutokea kwa matukio hayo na, kama ndivyo, kurekebesha kama ni lazima, mapungufu hayo kuhusiana na
   - (i) uchovu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti;
   - (ii) vifaa vya kazi;
   - (iii) uendeshaji wa kifaa cha kinga;
   - (iv) taratibu zilizopo;
   - (v) mpangilio wa mfumo wa SCADA; na
   - (vi) utendaji kazi wa mfumo wa SCADA.

(b) Mwenye leseni atajumuisha mafunzo yaliyopatikana kutoka "Best International Electricity Industrial Practices".

Mpangilio wa

92. Mwenye leseni atahakikisha kuwa mpangilio

chumba cha udhibiti

wa chumba cha udhibiti ina vipengele vifuatavyo:

(a) kina nafasi ya kutosha ya kufanyia kazi na kinazingatia asilimia 5 na 95 ya utumiaji;
(b) kinatokana na uchambuzi wa kazi zitakazo fanyika, kama uchambuzi wa kazi zinazohusiana au uchambuzi wa madaraja ya kazi;
(c) kina milango ya dharura ambayo inawezesha matumizi ya hadi asilimia 99;
(d) kina sehemu na milango inayowezesha waendeshaji wenye ulemavu kuingia na kutoka;
(e) mpangilio huu utatumika pia ikiwa kuna vyumba vingine vya udhibiti vinavyofanya kazi kwenye mfumo huo huo ili kuhakikisha uthabiti;
(f) mahusiano yote ya uendeshaji kati ya waendeshaji wa chumba cha udhibiti yanazingatiwa kubuni michoro;
(g) mawasiliano kwa maneno au pasipo maneno hayatakatazwa na mpangilio uruhusu kufanya kazi kwa pamoja;
(h) mpangilio wa chumba cha udhibiti uruhusu mgawanyo wa majukumu na mahitaji ya usimamizi;
(i) mpangilio uwe wa kuleta ufanisi chini ya kiwango cha juu au cha chini cha wafanyakazi;
(j) upatikanaji wa wafanyakazi wote ufikiwe kukiwa na usumbufu mdogo kwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti;
(k) ikiwa nafasi za usimamizi zitasababisha ongezeko la mzunguko wa watu, nafasi hizo zitawekwa karibu na milango ya kuingilia.
(l) umbali kati ya sehemu za kazi uhakikishe kuwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti hawaingiliani katika maeneo yao ya kazi;

(m) umbali wa chini kati ya sehemu za kazi utakuwa angalau milimita 3000;
(n) nafasi ya kutosha inabidi itolewe ili uendeshaji mitambo bila kukusudia wakati wa kufanya matengenezo hautawezekana;
(o) nyuma ya vifaa vya paneli kuwe na maelezo sahihi yanayotakiwa ili kupunguza uwezekano wa kutokea makosa ya kibinadamu.

Mazingira ya joto

93. Mwenye leseni atahakikisha kuwa joto na mzunguko wa hewa katika chumba cha udhibiti vinaweza kurekebishwa kufikia viwango vinavyokubalika katika sekta ndogo ya umeme.

Mazingira ya kuona

94. Mwenye leseni atahakikisha yafuatayo;

(a) mwanga wa taa kwenye chumba cha udhibiti hautakiwi kuweka vivuli katika vitengo vya kuonesha picha au sehemu nyingine inayong'aa ambayo inahitaji kufuatiliwa;
(b) mwanga wa taa katika chumba cha udhibiti uwe wa kiwango kati ya 500-800 lux;
(c) hakuna mtikisiko kwenye taa za utepe; na
(d) madirisha kwenye chumba cha udhibiti hayatakiwi kusababisha vivuli katika sehemu zinazo ng'aa kwahiyo kuna ulazima wa kuchukua hatua za kukinga mionzi ya jua.

Hali ya usikivu

95. Kila mwenye leseni atahakikisha kuwa-
(a) iwango cha kelele ndani ya chumba cha udhibiti inarekodiwa na kiwango kisizidi 85 db (A) siku nzima ya kufanya kazi;
(b) kelele ya muda mrefu au kelele za masafa ya chini zaidi au ya juu zaidi inabidi ziepukwe; na
(c) viwango vya kelele havitakiwi kuingilia kati mawasiliano, ishara za onyo na utendaji wa

akili.

Onyo la hatari

96. – (1) Mwenye leseni atahakikisha kuwa wafanyakazi wote na wakandarasi walioko sehemu za kazi wanaufahamu wa kila aina ya onyo la hatari, na wanaelewa njia za kutumia kushughulikia tatizo hilo hasa kama kisababishi cha onyo kina uwezekano wa kuwaathiri wao.

(2) Onyo la hatari liwe na uwezo wa kujiweka upya moja kwa moja kama tatizo lililosababisha kengele ya hatari limerekebishwa.

(3) Ujumbe wa onyo uwasilishwe kwenye fomati maalum, kuzingatia mikataba iliyopo.

(4) Ujumbe wa onyo unatakiwa kumjulisha kwa uwazi zaidi mwendeshaji wa chumba cha udhibiti sababu zilizosababisha tukio hilo.

(5) Kufuatia tukio hilo hatua za kuchukua kushughulikia tatizo hilo lazima zijulikane wazi kwa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti.

(6) Ukokotoaji wa maonyo ya hatari yasizingatie zaidi rangi peke yake, kwani waendeshaji wa chumba cha udhibiti ambao hawawezi kutofautisha rangi watashindwa kutambua kile kinachoonyeshwa na onyo la hatari.

(7) Ishara za onyo zinatakiwa ziwe angalau 10db (A) juu ya kelele za kawaida ndani ya chumba cha udhibiti.

(8) Onyo la hatari lisizuie mawasiliano ya uhakika ndani ya chumba cha udhibiti.

(9) Kitabu cha kumbukumbu ya matukio ya maonyo ya hatari lazima kiandaliwe kwa ajili ya uchunguzi wa matukio.

(10) Ubunifu wa mfumo wa utoaji onyo la hatari lazima uzuie kisingizio na mafuriko ya maonyo ya hatari.

Andiko

97. Mwenye leseni atahakikisha kuwa lugha inayotumika lazima iweze kueleweka kwa urahisi na

mwendeshaji wa chumba cha udhibiti.

Lebo

98. –(1) Mwenye leseni atahakikisha kuwa uwekaji lebo unafanyika kwa uthabiti pande zote za mitambo.

(2) Uhusiano kati ya lebo na mitambo inayozungumziwa lazima ijulikane wazi.

(3) Lebo ziweze kusomeka kwa urahisi.

(4) Ufupisho wa maneno utumike pale inapohitajika.

Vifaa vya kuonyeshea

99.- (1) Mwenye leseni atahakikisha kuwa vifaa vya kuonyeshea ni sahihi kwa aina ya taarifa zinazotakiwa kuonyeshwa.

(2) Vifaa vya kuonyeshea viwekwe kwenye makundi kwa mpangilio sahihi ili kuboresha usajili wa mawimbi.

(3) Kazi ya upangaji na mbinu za uchambuzi zitafanyika ili kuthibitisha mpangilio bora zaidi kwa uoneshaji na vifaa husika vya uthibiti.

(4) Uhusiano kati ya udhibiti na vifaa husika vya kuonyeshea unakuwa bayana kama ifuatavyo:

Uthibitisho wa utiifu

100. Kama kutakuwa na ombi, mwenye leseni atawasilisha kwenye Mamlaka taratibu za kijimenejimenti za chumba cha udhibiti.

Utiifu na Kupotoka

101. Mwenye leseni atahifadhi kwa ajili ya kufanya uhakiki wakati wa ukaguzi yafuatayo:

(a) taarifa ambazo zinathibitisha utiifu kwa matakwa ya sehemu hii;

(b) nyaraka kuthibitisha kwamba kupotoka kokote kutoka kwenye taratibu zinazotakiwa na sehemu hii ulikuwa wa lazima kwa ajili ya uendeshaji salama wa miundombinu ya umeme.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI YA JUMLA

Mpango wa kusitisha uendeshaji wa miundombinu ya umeme

102. –(1) Mwenye leseni ndani ya kipindi si zaidi ya miezi sita kabla ya leseni kumaliza muda wake na kutokuwepo kwa nyongeza ya muda wa leseni au maombi mapya au uhamisho wa leseni, kuwasilisha kwenye Mamlaka kwa kupata idhini, mpango wa kusitisha uendeshaji wa miundombinu ya umeme ambao utakuwa na-

(a) utaratibu wa kuondoa mitambo, usafirishaji mitambo nje kama upo, na uondoshaji wa vifaa vilivyobaki; na

(b) maelezo ya jinsi ya kurudisha upya ardhi na maeneo ya karibu katika hali yake ya zamani na mamlaka zinazohusika kujiridhisha na hatua hiyo.

(2) Mwenye leseni, baada ya muda wa leseni kuisha na kutokuwepo na maombi mapya ya muda wa leseni au nyongeza, atatekeleza mpango wa kufunga miundombinu ya umeme kama ilivyoelezwa kwenye kanuni ndogo (1).

(3) Mwenye leseni, endapo miundombinu ya umeme haitaondolewa kama inavyotakiwa chini ya kanuni ndogo (2) atawajibika kulipa tozo au adhabu yeyote ambayo imetolewa na mamlaka husika

Kusitisha uendeshaji wa mitambo wakati wa kufuta leseni

103. Bila kujali masharti ya kanuni zilizotangulia, mwenye leseni, endapo leseni yake itasitishwa na hakuna leseni nyingine ya kuchukua uendeshaji wa mitambo ya umeme, atawajibika kufunga uendeshaji wa mitambo ya umeme kwa kutumia vigezo vya utendaji kazi bora na wa busara.

Makosa

104. Mtu ambae atakiuka masharti ya Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani

atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua miaka miwili au vyote.

Kufuta TS. NA. 287 la 2019

105. Kanuni za shughuli za uzalishaji, upelekaji na usambazaji wa Umeme za Mwaka 2019 zinafutwa.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 74(1))*

**FOMU YA MAOMBI YA MTEJA WA UMEME**

| Na. | MAELEZO | IJAZWE NA MWOMBAJI |
|---|---|---|
| **1.** | Mambo ya Kawaida | |
| | Jina la Mwombaji | |
| | Namba ya cheti cha usajili | |
| **2.** | Anuani ya Mwombaji | |
| | Anwani ya Mwombaji | |
| | Anuani ya Makazi: kitalu Na., Namba ya Nyumba, Barabara | |
| | Anuani ya Posta | |
| | Kata/Mji | |
| | Wilaya | |
| | Mkoa | |
| | Simu ya mezani: | |
| | Nakushi: | |
| | Namba ya simu ya mkononi: | |
| | Barua pepe | |
| **3.** | Jina la Msambazaji | |
| | Anuani ya mahali: Kitalu Na., Namba ya Nyumba, Barabara | |
| | Anuani ya Posta: | |
| | Leseni ya Umeme: | |
| | Tarehe ya kwisha kutumika ya leseni: | |
| 4. | Mahitaji ya kitaaluma | |
| | Mahitaji ya umeme wa mwombaji (mw) | |
| | Nguvu ya umeme(kv) | |
| | Sahihi ya Mwombaji | |
| | Jina: | |
| | Sahihi | |
| | Wadhifa: | |
| | Tarehe: | |

Dodoma,
26 June, 2023

JAMES A. MWAIMYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*